# *Ni Nini Hiyo Uliyo Nayo Mkononi Mwako?*

(Asante sana, ndugu. Je, hili linapaswa kuwa shada langu la maua? Asante.)

2 Habari za jioni, marafiki. Nina furaha kuwa hapa usiku wa leo na nina furaha sana kwamba sote tunaweza kuwa huku nje. Namshukuru Bwana mwema kwa ibada Zake za ajabu jana usiku. Kusikia . . . Ni mara ya kwanza nimepata fursa ya kuwa miongoni mwa watu ku—kuwahubiria namna hiyo kwa muda mrefu na kuwahudumia.

3 Na jana jioni, nilipokuwa nikitoka, yule mvulana aliniambia, akasema, hawapendi mimi kuwa na mkutano wa aina hiyo kushuka chini kuwawekea watu mikono; wanawazia tu labda . . . Walisema wanapoitwa kutoka jukwaani huwa ni asilimia mia moja. Kisha kasema, "Unaliamini tu neno la watu kwake, wakati huo."

Nikasema, "Vema, wanayo imani, wanaamini."

4 Ndipo nilipokuwa nikishuka chini kati ya viti vya magurudumu, nilifikiri ilikuwa ni Billy akitembea mbele yangu. Basi ikatokea niligeuka upande kuangalia: haikuwa Billy, ilikuwa ni Yeye. Ndipo nilipoinuka, basi Bwana akaanza kutabiri, na kusema, "Kutakuwako na wengine kwenye viti vya magurudumu ambao watapitia kwenye kusanyiko; wengine watoke nje."

Huyo mvulana akasema, "Hilo litatukia?"

5 Nikasema, "Wewe tazama tu uone." Na hapo jana usiku . . . Hiyo ni kweli. Hao ni watu watano waliopooza kutoka kwenye viti vya magurudumu juma hili. Hilo ni jambo la ajabu analofanya Bwana wetu. Ninaamini atatenda makuu . . . zaidi ya hayo usiku wa leo, sivyo? Tunaamini ya kwamba atatenda.

6 Sasa, kesho usiku, kwa kuwa ni kumalizia kwa ibada hii . . . Mmekuwa wazuri sana kwetu, nanyi mkatoka na kuketi katika hali ya hewa wakati kulikuwa na baridi na mvua. Nanyi mmekuwa wazuri sana, sana, na sikuzote tutawakumbuka. Nami nimekuwa na namna fulani ya mapambano ambayo ni . . . Ninyi . . . Ni vema mlikuwa wazuri, kwa sababu si kawaida mimi kuzungumza na watu hivi au kuhubiri, na kisha kufanya wito wa madhabahuni na kadhalika.

7 Ndugu Moore kwa sababu fulani hakufika, naye Ndugu Arganbright hakufika, lakini Ndugu Thom kutoka Afrika Kusini, namtakia heri, alikuwa mahali fulani hapa, nilimsikia

akisema, “Amina,” muda mfupi uliopita. Huyu hapa anarudi. Na hiyo ilikuwa . . .

8 Haimkini huyo si yule mvulana mdogo aliyeitwa William Branham? Naam, jamani. Ndio mara ya kwanza nimekuona, mwanangu. Wewe ni mvulana mzuri. Sasa natarajia kukuona nyumbani kwangu karibuni sana. Unaona? Naam, hilo ni jema sana. Najua nyote mnayafurahia mahubiri ya Ndugu Thom. Pengine atakuwa kwenye kanisa fulani hapa kesho.

9 Ndugu Beeler anayeketi hapa, labda atakuwa akihubiri mahali fulani asubuhi pia. Hawa wavulana wengine hapa, nadhani wamepangiwa makanisa fulani.

10 Sasa, ninyi mlio hapa na katika ibada, wageni waliotutembelea, mbona, ta—tafuteni kanisa zuri mpate kwenda kanisani asubuhi. Wahudumu hawa wote hapa, wanawakilisha makanisa haya ya full Gospel kote huku Atla-. . ., au, Macon hapa. Nao wangefurahi kuwa nanyi kanisani mwao.

11 Na hata sijapata kukutana na yeyote wa hao ndugu ila maskini Ndugu Palmer hapa. Huenda nilipeana mikono na baadhi ya ndugu hawa. Lakini kama wote ni kama Ndugu Palmer, wao ni watu wazuri, ninawaambia hilo, wao ni wazuri sana, ndugu wazuri tu.

12 Na sasa, tunatumaini kuwa kesho kutakuwa na ibada nzuri kote . . . kote nchini. Simama kwenye wajibu wako wa kazi kesho; sasa, kesho asubuhi nenda kwenye shule ya Jumapili. Basi hebu tuone, nadhani kesho alasiri ibada ziko hapa. (Hiyo ni kweli? Kesho alasiri? Kesho usiku? Vema, waliibadilisha mpaka . . .) Kisha ibada . . . (Tayari umeitangaza, nadhani? Vema.) Ibada ziko hapa kesho usiku. Vema. Sasa, Bwana abarikiwe ndilo ombi letu aminifu.

Sasa, kwa ajili ya somo ili kutafakari kwa muda kidogo. Nasi tunataka kusema tena: tunamshukuru sana Bwana mpendwa kwa yote ambayo amefanya.

13 Sasa, ninaamini ya kwamba katika mkutano wowote wa Marekani wa siku nyingi hivi, kupata watu watano waliopooza kuponywa katika mkutano mmoja, ninaamini hilo karibu ni—ni kubwa tu kadiri Bwana alivyotutendea mwaka huu mzima. Na sasa, katika Afrika, ama baadhi ya nchi zingine, huko India, ama kitu kama hicho, ni tofauti. Lakini hapa Marekani, kwa sababu kuna ibada nyingi zinazoendelea, na jambo moja, kamwe hatukai usiku kumi, kwa kawaida huwa tu huko angalau kuanzia siku tatu hadi tano usiku kisha tunaenda. Kwa hiyo ninasema tu kwamba, kwa hilo, mnaweza kuona au kujua kwamba ninaamini mna imani kuu, nami nina furaha sana.

14 Walisema wengi wa watu wamekuwa wakitoa ushuhuda. Ndugu Wood na hao wengine walikuwa wakiniambia leo juu ya watu kushuhudia, na kila aina ya magonjwa na kila kitu, yameponywa. Na watu kadha kwenye machela, siamini tuna

kitanda ila kimoja hapa usiku wa leo. Mungu ameyamaliza tu magonjwa ya vitanda na kila kitu. Si ni ajabu hiyo?

15 Aisee, na jambo lingine, jana jioni, wakati nikija jukwaani, yapata mmoja wa wa kwanza kuja alikuwa na—na ugonjwa wa kusikitisha. Nimeona usiku wa siku chache zilizopita mwanamke aliyeketi na mtoto mchanga mwenye kichwa kilichojawa maji, nao huo hakuna kitu kinachoweza kufanywa kwake kwa njia ya utafiti wa matibabu, kilichopo katika utafiti wa kisayansi kuwasaidia hawa jamaa wadogo. Hawajiwezi kabisa. Na maskini mama huyo alikuwa makini sana, akimbeba jamaa huyo mdogo usiku baada ya usiku, huku yeye akilia. Niliendelea kumtazama maskini mtoto huyo, na niliweza kuona shida ilikuwa nini. Na mara nyingi maono hunena; hata sisemi lolote kuyahusu.

16 Jamaa huyu ametoka kunipigia simu dakika chache tu zilizopita, nami nilikutana naye katika m—mgahawa hivi majuzi usiku, na huko Bwana akaniambia shida yake. Alinipigia simu, akasema, "Unajua, kwa sababu umeninii . . . Nimekuona," kasema, "nimepata nafuu zaidi." Nikamwambia tatizo lake; nusura azimie. Mwajua . . . Na kwa hiyo yeye . . . Jambo ndilo hilo. Inakubidi tu kuangalia; utaona litatokea tu kwa vyovyote vile. Kwa hivyo, sio sana sana kama wanajua chochote juu yake, mradi tu unajua . . . kati ya . . . kwamba Mungu amesema itakuwa sawa. Kwa hiyo hilo—hilo latosha, unaona. Si wazo la kwamba tunataka watu wajue, mradi tu Mungu anasema hivyo, vema, amina, achana nalo tu, na ikiwa unafikiri kuwatia moyo kidogo kungewasaidia, basi kwa kawaida unasema kitu.

17 Lakini mtoto huyu mchanga akapitia jukwaani, kichwa kikubwa mno kilichojawa maji, ameegemea maskini mama mdogo, aliyechoka. Basi nilipomwekea mikono mtoto huyo, niliona ile Nuru ikikizunguka moja kwa moja kichwa cha huyo mtoto, nami ni—nikajua kitu fulani kitatokea. Kwa hiyo nikamwuliza huyo mama kama angempeleka mtoto nyumbani. Na nilijua ya kwamba jambo fulani lilimpata wakati huo, kama ningekuwa na kitu cha kumthibitishia mama huyo. Lakini nikamwambia, nikasema, "Wewe mpeleke huyo mtoto nyumbani." Naye aliishi nje ya mji; ninaamini Yeye alimwambia, mahali fulani, kama maili mia moja. Anasafiri kama maili mia mbili kila usiku kumleta huyo mtoto.

18 Ndipo alipofika nyumbani, nilisema, "Weka kamba ndogo kuzunguka kichwa chake na uipime hiyo kamba, na kisha uikate kamba hiyo; halafu umfungie hiyo kamba moja kwa moja tena kesho yake usiku, kesho usiku, na uniletee hicho kipande cha kamba kuonyesha kichwa cha huyo mtoto kimepungua kiasi gani." Katika ish- . . . na hii itakuwa kama saa kumi na nane au ishirini, basi hii hapa kamba yapata inchi moja na nusu ya ile kamba, ambapo kichwa cha huyo mtoto kilipungua katika yapata saa kumi na nane. Sijui kama huyo mama yuko hapa

mahali popote na huyo mtoto usiku wa leo . . . Loo tayari yuko . . . Huyu hapa mama. Hiyo ni kweli, vema. Mungu akubariki, dada.

19 Sasa, sababu ya mimi kufanya hivyo, Dada, ilikuwa hii, ili upate kutiwa moyo. Nimeombea mambo mengi ambayo si—si—sikuyapata, lakini siamini, nikiwa mbele ya Muumba wetu usiku wa leo, kwa uaminifu kabisa, nilimwomba Mungu jambo lolote kwa uaminifu hivyo, pasipo Yeye kunipa au kuniambia kwa nini hangeweza kunipa. Mnaona?

20 Sasa, hiyo inchi moja na nusu ya huyo mtoto, kichwa cha mtoto huyo kimepungua katika yapata saa kumi na nane au ishirini, hiyo ni kuwatia moyo. Mnaona? Sasa, endelea tu kuamini. Unaona? Sasa, ita—itafanya hivyo kwa yapata saa sabini na mbili. Kisha utaona, wewe endelea kukata kamba yako. Itakoma; inaweza kuwa mbaya zaidi kwa muda kidogo. Haijalishi nini kitatokea, wewe endelea tu kuamini. Unaona? Na maadamu utaidumisha imani yako . . .

21 Sasa kumbukeni, pepo mchafu anapomtoka mtu, hutembea mahali pasipo na maji na kurudi tena pamoja na roho zingine saba mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa; na kama akiweza, ataingia na kuchukua mamlaka, ndipo hiyo hali itakuwa mbaya zaidi. Lakini ikiwa mwenye nyumba hayupo, ambaye ni imani yako, kumzuia . . . Kamwe usimshambulie. Atakushambulia pia. Kataa tu; mpuuze tu. Hivyo tu. Endelea tu. Sema tu imekwisha; hilo latosha kabisa. Naye mtoto wako atakuwa mzima. Sasa, Bwana akubariki.

22 Sasa, usiku wa leo . . . Ninalipenda tu Neno. Hivi hamlipendi Neno? "Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno." Ninataka tu kusoma somo dogo tu hapa usiku wa leo, kwa ajili ya muktadha kidogo, nasi tunataka kulisoma kutoka katika Kutoka mlango wa 4, Bwana akipenda, na kuanzia kifungu cha pili. Tutasoma labda kifungu cha pili na labda sehemu ya 3.

> *Bwana akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo.*
>
> *Akamwambia, Itupe chini; Akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake.*
>
> *Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; Naye akanyosha mkono wake, akamshika* mkia, *naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake:*

23 Sasa, twaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi mafupi tunapozungumza na Mwandishi wa *Hiki*, kisha tuziombee leso hizi hapa?

24 Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunashukuru sana kukusanyika hapa tena usiku wa leo chini ya vivuli vya anga hii, kutazama juu Mbinguni kunakotoka msaada wetu; msaada wetu unatoka kwa Bwana. Tuna furaha sana kujua kwamba Yeye yu

hai na anatawala leo wala hajaliacha kanisa Lake bila shahidi wa kufufuka Kwake.

25 Nasi tunashukuru sana usiku wa leo kwamba sisi, kama vile wana wa Israeli, tutakaozungumza habari zao, ikiwa ni mapenzi Yako, katika dakika chache, jinsi walivyopita huku wamelemewa na mizigo yao, na kuchungulia ndani ya jeneza la Yusufu, na kuiona hiyo mifupa ikiwa imelala pale, wakijua ya kwamba Mungu alikuwa ameahidi kupitia kwa nabii ya kwamba siku moja wangeondoka. Basi usiku wa leo kama mfano wa Yusufu, Mfalme wa ufanisi, Bwana Yesu alifufuka katika wafu naye yuko hai usiku wa leo hapa miongoni mwetu kama ushahidi wa Kiungu kwamba siku moja tutaondoka, kutoka katika ulimwengu huu wa taabu na dhambi, na alipo Shetani na nguvu zake zote; ndipo tutakuwa huru kutoka kwake milele.

26 Sasa, Bwana, tunapoyatafakari maneno haya, naomba Roho Mtakatifu aje, aingie katika Neno, na jalia aligawanye kwa kila moyo, sawasawa na mahitaji yetu usiku wa leo. Na jalia tuseme, kama wale waliokuja kutoka Emau, wakati alipoumega mkate na kufanya jambo tofauti kidogo na lile mhudumu wa kawaida alifanya katika siku hizo. . . Alifanya hivyo kwa njia ambayo Yeye peke Yake angeweza kufanya. Na, Baba, tunaomba usiku wa leo ya kwamba atafanya jambo lisilo la kawaida ambalo hatulioni kila siku katika kila ibada ya kidini. Ili tu watu wapate kujua ya kwamba Bwana Yesu yeye yule yu hai kutoka kwa wafu usiku wa leo, akitembea huku na huko miongoni mwa watu, akifanya mambo yale yale aliyofanya wakati huo. Tujalie, Baba.

27 Leso hizi zilizowekwa hapa, zinawakilisha maskini watoto wadogo, wagonjwa, baba, mama, watu wengi waliolala huko nje, wakiteseka, kwa sababu ya magonjwa na ukandamizaji wa ibilisi. Na, Baba, huku mikono ikiwekwa juu yazo kwa maombi, moyo wangu wote, ninaomba ya kwamba utanisikia, Bwana, na ujue unyofu wa moyo wangu, tunapokemea kila roho mchafu, kila nguvu za pepo zinazowafunga watu ambao leso hizi zitawekwa juu yao. Ndipo leso hizi zitakapowekwa juu yao, na wafunguliwe, Bwana, na waende zao wakifurahi, na Shetani afungwe na kutupwa katika giza la nje. Tujalie, Baba. Tusaidie sasa katika sehemu ijayo ya ibada hii, kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

28 Sasa, tunapotafakari kwa dakika chache hapa juu ya Neno la Bwana, ninatumaini ya kwamba kila mtu ataninii tu. . . Nitajaribu kuharakisha, kwa hivyo, najua upepo unavumisha baridi kidogo na kwa wagonjwa, basi nitajaribu kuharakisha. Na labda kesho usiku kutakuwa na joto zaidi na tutakaa kwa muda mrefu zaidi.

29 Hivi majuzi tukitoka tukiangalia juu, mimi pamoja na Bw. Wood tulikuwa tukishuka barabarani nami nikaona wale wakulima maskini huku mahindi yao yamekusanywa

tu (nilikuwa nikilima kidogo, pia.), na matikiti maji na kila kitu, pamba inakauka. Nikaenda nyumbani, nikasema, "Mungu Mpendwa, najua tuna ibada ya hadharani, lakini tafadhali wapelekee watu hao mvua, kwa sababu kweli wanahitaji mvua." Nami nikawaza tu juu ya ukuu wa Bwana Yesu, jinsi alivyoiruhusu mvua kunyesha kufikia kwenye hiyo ibada, ikatulia tulipokuwa na ibada, kisha kuwalowesha kwelikweli jana usiku; akaisimamisha kwa ajili ya usiku wa leo. Loo, jamani. Jinsi Yeye alivyo wa ajabu. Anajua tu jinsi ya kufanya hivyo, sivyo? Nasi tunampenda tu sana kwa sababu hiyo. Anastahili sifa zote tu.

30 Sasa, usiku wa leo, nataka kuzungumza kwa muda mfupi tu juu ya somo la *Ni Nini Hiyo Uliyo Nayo Mkononi Mwako?*

31 Sasa, ninii . . . muktadha wetu usiku wa leo unahusu Musa, mtu ambaye alitumiwa na Mungu, huko nyuma, kuwakomboa wana wa Israeli kutoka chini ya utumwa wa Misri. Nao watu wengi, usiku wa leo, wa Mungu, wako utumwani.

32 Ninamwangalia ameketi hapa, mama aliye na mvulana mdogo, inaonekana kama labda miguu ya—yake midogo huenda imeenda kombo ama chochote kile. Analala karibu na mama yake. Jamaa mdogo anayeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, mtoto mdogo, labda amekuwa na polio ama chochote kile. Maskini mguu wake umefungwa kwa magango.

33 Ninaona msichana mdogo ameketi hapa msichana mdogo mrembo, anaonekana yuko katika ujana wake bado, na maskini baba mzee aliyepinda kwenye kiti cha magurudumu, namna *hiyo*. Huo ni utumwa. Shetani amefanya hivyo.

34 Huyu hapa ndugu mweusi ameketi hapa. Mtu fulani ameketi karibu naye, akimshikilia na, au, karibu naye. Basi angalia tu utumwa ambao Shetani amewaletea.

35 Naye Mungu ananinii tu . . . anakupenda kama vile Yeye alivyowapenda wale Waebrania. Na wakati . . . Mungu alimtuma Musa huko chini kwa sababu alikuwa ameahidi kwamba angekuja na kuwakomboa kwenye utumwa huo.

36 Naye Mungu ameahidi katika siku hizi za mwisho ya kwamba angemtuma Yesu Kristo, Roho Mtakatifu, katikati yetu na angewaweka huru wagonjwa wote na wanaoteseka. Kwa maana imeandikwa, Maneno ya mwisho aliyosema kabla ya kuondoka hapa duniani, alisema, "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Umbali gani? Ati wakati wa mitume? Ulimwenguni mwote; Injili haijawahi kufika ulimwenguni mwote bado. "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; naye asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; watashika nyoka; au wakinywa

vitu vya kufisha havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

37 Yesu, akipokelewa juu Mbinguni; agizo la mwisho alilowahi kulitolea kanisa lilikuwa ni kuwaponya wagonjwa. Agizo la kwanza alilowahi kulipatia kanisa lilikuwa ni kuwaponya wagonjwa. Akawachagua watu Wake sabini na watu Wake kumi na wawili, akawatuma, na kuwapa mamlaka juu ya pepo wachafu, kuwatoa pepo, na kuwaponya wagonjwa, agizo la kwanza. Agizo la mwisho lilikuwa, enendeni ulimwenguni kote mkawaponye wagonjwa.

38 Juu ya Maandiko hayo, najua wanatheolojia wengi wameyajadili na kusema miongoni mwao, kwamba hiyo Marko 16 ambapo nilikuwa nikinukulia, kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea haikuvuviwa.

39 Inanikumbusha, siamini mimbara ni mahali popote pa kufanyia mizaha wala siamini katika mizaha; dumisha mimbara ikiwa safi; mizaha ni ya huko nje. Lakini hili lilikuwa nukuu dogo tu ambalo lilikuwa la kweli, nalo linaonekana kama linaweza kuwa ni mzaha, lakini sivyo.

40 Kulikuwa na maskini jamaa mmoja katika sehemu yetu ya nchi, ambaye alikuwa na wito wa huduma. Mama yake alikuwa bikizee mzuri sana, naye alimpeleka kwenye seminari apate kuwa mhudumu. Basi alipokuwa ameondoka, mbona, kwenda chuoni na seminari, akijifunza jinsi ya kuhubiri na kadhalika, vema, ninii...mama yake alishikwa na ugonjwa, mgonjwa sana; alishikwa na nimonia. Basi wakamwita daktari, naye akampa, bila shaka, yote ambayo angeweza kumpa. Wala hangeweza kumeza penisilini; alikuwa na mzio nayo. Kwa hiyo alikuwa akimpa dawa ya salfa na vitu vingine; wala haikusaidia. Yule mwanamke, vema, mapafu yake yalikuwa yakimsonga kabisa, naye alikuwa mahututi. Kwa hiyo wakampigia simu mwanawe na kumwambia akae chonjo, maana walidhani mama yake angekufa mara moja na ikawabidi...wanamtaka arudi nyumbani. Alikuwa umbali wa maili nyingi.

41 Lakini kwa ghafla, mbona, kulikuwako na msichana aliyeishi hapo chini pembeni, mfuasi wa misheni ya Full Gospel, aliyeishi pembeni ambaye aliamini katika uponyaji wa Kiungu. Basi akapanda kwenda kumwona yule bikizee, akasema, "Dada," akasema, "mchungaji wetu anaamini, pamoja nasi, huko chini kwenye kanisa letu, ya kwamba Yesu alikufa ili kuwaponya wagonjwa. Na kama hungejali, kwa nini usimruhusu mchungaji wetu aje akuombee? Labda Mungu angejibu maombi yake na kukuponya."

Akasema, "Hilo litakuwa zuri sana. Mleteni huku." Kwa hiyo huyo mwanamke...mwanamume huyo akaja, naye akamwombea, ndipo akapona.

42 Yapata mwaka mmoja baadaye, mwanawe akarudi nyumbani, nao walikuwa wakijadili mambo baada ya kukutana. Akasema, "Mama, jambo lingine," akasema, "sijawahi kusikia kile hasa daktari alikupa hata ukapona upesi sana, uliposhikwa na nimonia, nilipokuwa nikijiandaa kuja."

Akasema, "Loo, mwanangu," akasema, "Nilisahau kukwambia." Akasema, "Unajua ilipo ile misheni ndogo huko chini pembeni?"

Naye akasema, "Naam."

43 Kasema, "Unajua, huyo mama alikuja hapa na kuniambia mchungaji wake aje akaniombee." Kisha kasema, "Unajua, alikuja na kusoma sehemu ya Biblia katika ninii. . . Marko mlango wa 16, na kusema, 'Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.' Unajua, Bwana akaniponya mara moja?"

44 "Mbona," akasema . . . yule mvulana akasema, "sasa sikiliza, mama," kasema, "sasa, hao watu hawana elimu." Kasema, "Unaona, hawaelewi." Kasema, "Sisi. . . " Kasema, "Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu." Kasema, "Hakuna kitu kama hicho katika Biblia." Kasema, "Huo ulikuwa katika siku zilizopita." Kasema, "Sasa, katika seminari, mbona, tulijifunza ya kwamba Marko 16, kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea, haijavuviwa."

Maskini yule mama akasema, "Vema, Haleluya!"

Naye akasema, "Mama. Mbona," akasema, "unajifanya kama hao watu."

Naye akasema, "Naam, utukufu kwa Mungu!"

Akasema, "Vema, mama, kwani una shida gani?"

45 Kasema, "Nilikuwa tu nikiwazia: kama Bwana angeweza kuniponya kwa Neno lisilovuviwa, angeweza kufanya nini hasa na *Lile* lililovuviwa kweli?" Ikiwa sehemu hiyo haijavuviwa? Kwa hivyo hiyo ni kweli. Ninaamini Yote imevuviwa. Kila sehemu Yake. Na yote ni kwa ajili yetu, kila sehemu ni yetu.

46 Hatuna haja wala kukosa chochote. Mungu ametupa kila kitu tunachohitaji katika safari hii. Kimetolewa kwa ajili yetu papa hapa. Loo, kamwe . . . Kila wakati mtu anapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, Bwana anampa kitabu cha hundi cha ku- . . . cha kumtosha safarini mwake; na kila sehemu ya chini ya hiyo hundi, kwa ajili ya baraka yoyote ya ukombozi, imetiwa sahihi, Jina la *Yesu*. Ijaze tu kisha uitume. Angalia kama Yeye hataiheshimu. Hiyo ni kweli. I—itume tu huko. Hiyo, hizo amana, tayari ziko mle ndani. Iliwekwa pale Kalvari: "Kwa maana alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu: adhabu ya amani yetu juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Yote imetiwa sahihi katika Damu Yake. Yote yamekwisha. Yeyote . . . "Atakaye, na aje." Na imethibitishwa.

Imethibitishwa hapa, ya kwamba amefufuka katika wafu na Yu hai miongoni mwetu usiku wa leo.

47 Yeye ndiye Mkombozi wetu sisi tulio utumwani. Mtu yeyote aliye utumwani, Yesu Kristo yuko hapa kuwakomboa usiku huu kama mtaamini. Sasa, siko hapa kuwakomboa, kwa kuwa nisingeweza kufanya hivyo. Sikutumwa kufanya hivyo. Nilitumwa kuihubiri Injili. Hakuna mengine. Kristo alikuja kukomboa.

48 Sasa, Musa, alipokuwa tu mtoto mchanga, ninii tu... Ilikuwa tishio kubwa huko Misri na walikuwa wakiwaua watoto wote wa kiume. Na papo hapo wakati Musa alipozaliwa, na mama yake, akimwona kuwa ni mtoto mzuri, hakuogopa tishio la Farao la kile alichokuwa akifanya na watoto wote.

49 Sasa, kama mtaona marafiki, kwanza kabisa, ninawatakeni mpate jambo hili kwa makini sana, kwanza kabisa, kwamba karama na miito havina majuto. Hiyo ndiyo husababisha shida. Mnaona? Usijaribu kuiga chochote; kuwa tu kile ulicho katika Ufalme wa Mungu. Ikiwa wewe ni kidole, kuwa kidole; ikiwa wewe ni pua, kuwa pua; jicho, kuwa jicho. Natumaini kidole changu kamwe hakitaamua kutokuwa kidole, kwa sababu si jicho. Hakika itanitoa kazini kwa muda. Kwa hiyo ndivyo hivyo, lazima sote tupate misimamo yetu na kuendelea. Lakini kundi lote pamoja ni Mwili wa Bwana Yesu Kristo, haijalishi ni nini.

50 Sasa, kuonyesha ya kwamba karama na miito havina majuto. Mwangalie Yesu; alikuwa Uzao wa mwanamke kutoka bustani ya Edeni. Alizaliwa Mwana wa Mungu. Musa, alikuwa mtoto mzuri alipozaliwa, naye alizaliwa kuwa mkombozi. Hangeweza kujizuia kuwa nabii. Mungu alimfanya hivyo wakati wa kuzaliwa kwake.

Mwangalie Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, yeye alikuwa ni "sauti ya mtu aliaye nyikani."

51 Angalia Yeremia, Yeremia 1:4, naamini. Mungu alimwambia Yeremia, akasema, "Nilikujua, na—na nikakutakasa, na kukuweka kuwa nabii wa mataifa, kabla hata hujaumbwa katika tumbo la mama yako." Sasa, huna budi kuamini katika kuchaguliwa tangu zamani na kujulikana tangu zamani, uninii tu, kuko.

52 "Karama na miito havina majuto." Hivyo ndivyo Mungu alivyoweka kanisani. Ninatofautiana kidogo na ndugu zangu wa Mvua ya Vuli hapo, kwenye hilo la kuwekea mikono, utekelezaji wa karama za kiroho. Naamini mlikosea hilo. Mnaona? Hiyo ni sawa, hatutaki kubishania hilo, lakini mimi ni—ninaamini mmekosea hapo. Mnaona?

53 Paulo na Timotheo, walitambua kwamba hiyo ni kweli, Timotheo, kuwa mhudumu na mtu mwenye kipawa. Tunafanya jambo lile lile katika kanisa la Kibaptisti na mengine yote,

tunapomwona mtu kama huyo, kumwekea mikono. Lakini sio kumpa karama ya kiroho, bali kumpa mkono wa kuume wa ushirika na baraka kuhudumu kwa karama ambayo Mungu amempa. Hiyo—hiyo ndiyo tofauti, mnaona. Na kwa hiyo ukijaribu kumpa karama, hivyo ndivyo mwanadamu hufanya, mnaona, wala kamwe haitafanikiwa. Hakika haijafanikiwa, na sidhani kama itawahi.

54 Sasa, lakini wakati Mungu amefanya jambo lolote, ni tofauti. Musa alitambua kwamba alikuwa Musa. Mungu, jinsi alivyomhifadhi na kumtunza. Na ndipo alipofikia umri mzuri, alifikiri watu hakika wangeelewa, wawe na nia ya kiroho kuelewa.

55 Sasa, kuna jambo ambalo laiti tungekuwa na wakati, kama haikuwa baridi sana, kulitafakari kwa muda mfupi tu: Watu walikosa kuelewa, sana! Ndipo alipomwua yule Mmisri, akidhani ya kuwa watu wangeelewa, watu wake mwenyewe, kwamba alitumwa kuwakomboa, lakini, hawakuelewa. Sasa . . .

56 Tunaona basi, ya kwamba alikimbilia nchi ya Midiani. Na huko akamwoa msichana Mkushi jina lake Zipora. Musa, hapo mwanzo, alikuwa na hasira kali sana. Tunajua hilo. Ilibidi Mungu aitoe ndani yake. Hivyo basi sisi . . . alimwoa msichana huyu na akawa mtumishi wa baba mkwe wake, kuchunga kondoo upande wa nyuma ya jangwa.

57 Siku moja, ninaweza kuwazia tu, nikimwona mzee huyu sasa mwenye umri wa miaka themanini. Alikuwa na watoto wawili waliozaliwa kwake huko juu. Na huyu hapa anashuka, sasa, akiwachunga kondoo, mchunga kondoo tu, mwanamume kutoka . . . aliyetoka nje ya mapenzi ya Mungu, na kumwua mtu, na huko nyuma, sasa, kama mchungaji wa kondoo.

58 Lakini kama Mungu ametangulia kuchagua jambo lolote, lina hakika tu kutimia, kadiri Mungu alivyo Mbinguni. Kwa hivyo litakuwa kwa vyovyote vile. Hakuna kitu duniani kinachoweza kumzuia Yesu Kristo kuja mara ya pili. Mungu ameamuru iwe hivyo. Hakuna njia ulimwenguni ambayo kamwe ungeweza kuusimamisha Ujumbe wa uponyaji wa Kiungu. Unaweza kupigana nao kadiri unavyotaka, lakini Mungu amekusudia kwamba unapaswa kwenda mbele, na unaendelea. Hiyo ni kweli. Haijalishi, mtu fulani . . . "Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Kwa hiyo jambo bora zaidi la kufanya ni kujiunga na mpango wa Mungu na kusonga mbele na kanisa, ndilo jambo bora zaidi ninalojua kufanya.

59 Hapa siku moja, nilikuwa juu kwenye Sanamu ya Uhuru na nikatoka nje kwenye mkono huo. Basi nilipochungulia nje kwenye dirisha lile, niliona kundi la shomoro waliokuwa wamekufa, wamelala kote huko nje. Ndipo nikamwambia yule kiongozi, nikasema, "Aisee, kuna nini? Mashomoro hao wadogo wa—wamekufa."

60 Akasema, “Bwana, kulikuwa na dhoruba jana usiku, nao maskini jamaa hao wadogo wakizunguka huku na huku, na kuingia kwenye taa za Sanamu hii ya Uhuru hapa. Basi badala ya kuzifuata hizi taa wapate usalama, walikuja na kuzigongesha bongo zao mle, wakijaribu kuzima hizo taa. Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikuwa wakijaribu kuzizima ndipo wakajiua katika jitihada.”

61 Nikasema, “Mungu asifiwe. Huenda wakawepo makafiri waliolelewa pamoja, wowote wale, wenye kushuku, na wasioamini, lakini kadiri unavyoigonga Taa ukaizime, kujaribu kuigonga Taa ya Mungu, utajigonga tu hata ufe na kuanguka chini kwa fedheha, nayo Nuru ya Mungu itamulika kote katika nyakati.” Hiyo ni kweli. Mungu atasonga mbele licha ya chochote mtu yeyote anachoweza kufanya. Jambo bora zaidi la kufanya ni kujiunga Naye na kuendelea mbele moja kwa moja na—na mtiririko wa Roho Mtakatifu.

62 Naye Musa, alipokuwa huko nyuma upande wa nyuma ya jangwa, siku moja, ninawazia kidogo amevunjika moyo, akienda zake, akifikiria juu ya kile kilichotukia huko Misri, na marafiki zake wote. Na hapa alikuwa amefunga ndoa katika jamii nyingine ya watu, na kuchunga kondoo za baba mkwe wake. Ilitokea alitazama kule, na akaona kichaka kikiwaka moto, na akawazia ilikuwa ni ajabu kwamba kile kichaka hakikuteketea kamwe. Kwa hiyo, Mungu alikuwa akijaribu kuuvutia usikivu wa Musa.

63 Nami najuaje, unajuaje, kama mkutano huu huku nje haujakuwa wa. . .Mungu ameuweka huku nje kuwamakinisha baadhi yenu ninyi watu mnaoishi katika makanisa haya hapa, bila kujua ya kwamba Mungu alifufuka katika wafu, na Yesu yu hai hapa usiku wa leo akiwaponya wagonjwa na wanaoteseka? Labda alikuleta hapa nje uone hawa viwete, na vilema, na watu waliopindika wakiinuka kutoka kwenye viti vya magurudumu na kuondoka, kuona Roho Wake akipitia katikati ya wasikilizaji na kuwarekebisha watu, na kuwakemea wenye dhambi hapa jukwaani, watakatifu, watu walioonekana watauwa, akija na kuwaambia mahali wanapotenda dhambi, na mambo yalivyo. Na kila Neno lake ni kweli isiyoweza kukosea. Unajuaje kwamba Mungu hajavutia usikivu wako ili kuja kutazama kitu kama hicho, ili nawe ugeuke pia? Si kuacha kanisa lako, bali kuachana na maisha unayoishi, na kumtumikia Mungu aliye hai katika kuzaliwa upya na kuzaliwa mara ya pili. Labda Mungu anafanya hivyo.

64 Musa akageuka, na alipokitazama kile kichaka kilichowaka moto, akaanza, akasema, “Vema, nitapanda nione tamasha hii ni ya nini.” Kwa kawaida Mungu hujifunua Mwenyewe katika moto.

65 Basi akageuka ili kuiona, ndipo Mungu akasema naye

kutoka katika kile kichaka na kusema, “Musa, vua viatu vyako, kwa maana mahali hapo uliposimama ni mahali patakatifu.”

Sasa, vipi kama Musa angalisema, “Sasa, Bwana nitakuwa tu na kicho Kwako, nitatoa kofia yangu, hilo litakuwa ni sawa vile vile”?

Mungu kamwe hakusema, “kofia yako,” alisema, “viatu vyako.”

Sasa, kama nitasema, “Vema, ninajiunga na kanisa; mimi si ni mwema tu kama huyo mtu mwingine?”

Mungu kamwe hakusema, “Kama mtu hajiungi na kanisa. . . ” Alisema, “Mtu hana budi kuzaliwa mara ya pili. Asiponinii . . . ”

Kasema, “Vema, ni—ninahudhuria kanisa zuri.”

66 Hiyo ni sawa, lakini hiyo siyo inayohitajika. “Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hataingia kamwe katika Ufalme.” Mungu ana mpango mmoja madhubuti, haidhuru kitu kingine chochote kinaonekana kuwa kizuri jinsi gani. Huna budi kujilainisha na Injili ya Mungu. Biblia inasema hivyo, na hilo ndilo jambo tunalopaswa kufanya.

67 Basi ilimbidi Musa kuufuata mpango wa Mungu, si kile Musa alichofikiri ni uchaji, bali kile Mungu alichokiita uchaji. Basi akaketi chini, akavua viatu vyake, akapanda juu. Akasema, “Nimeninii,” Yeye, “nimesikia kilio cha watu Wangu, nami nimeshuka, nami nitakutuma kule chini ukawakomboe.”

68 Mnajua Musa alilalamika. Akasema, “Sasa, tazama, mimi si mwepesi wa kuongea. Siwezi kuongea vizuri sana, na ulimi wangu ni mzito, na kadhalika.” Alianza kulalamika, ndipo Mungu akamwambia atamtuma Haruni. Ndipo alitaka kujua, akasema, kama angeweza kuuona utukufu Wake, angewaambia ni kitu gani kilitukia?

Mungu akamwambia Musa, “Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako?”

69 Sasa, chochote kilichokuwa karibu, Mungu angeweza kutumia chochote. Mungu angeweza kutumia kichaka. Lakini Musa alikuwa na kitu mkononi mwake. Akasema, “Ni fimbo.”

70 Akasema, “Itupe chini.” Naye akaitupa chini, na alipoitupa, ikageuka ikawa nyoka. Akaishika mkia; ikageuka kuwa fimbo tena. Naye Mungu akamwonyesha Musa kwa jambo hilo, yale ambayo angeweza kufanya, ya kwamba Yeye alikuwa angali ni Mungu aliye hai. Angeweza kuchukua ya asili na kuibadilisha kuwa ya kimbinguni. Angeweza kufanya chochote alichotaka, kwa maana Yeye alikuwa Mungu.

71 Musa akaokota fimbo ile mkononi mwake, akakimbia na kumchukua Zipora, mkewe, na kumketisha juu ya nyumbu, na kumweka mtoto kwenye kila nyonga. Akamkamata maskini

punda mmoja kwa hatamu na fimbo mkononi mwake, naye huyu hapa akishuka kwenda Misri kuwakomboa . . . watu milioni mbili.

72 Ungeweza kuliwazia hilo? Hilo lingekuwa jambo la kuhuzunisha jinsi gani. Mzee huyu, mwenye umri wa miaka themanini, mwenye ndevu nyeupe na nywele zikipepea namna *hiyo*, akifurahi tu na kushangilia, akipiga makelele, "Utukufu kwa Mungu," mke wake ameketi kwa kumtagaa nyumbu huyu, akiwa na mtoto mchanga kwenye kila nyonga, akishuka kwenda kuiteka. Ungeweza kuwazia hilo?

73 Unafikiri yale majeshi makubwa na askari wangesema nini siku hiyo? "Vema maskini yule mzee ameingia kichaa." Ulimwengu sikuzote huwazia hilo, bali yeye alikuwa na Neno la Bwana, Nalo lilipaswa kutimia. Alikuwa na ahadi ya Mungu. Naye alikuwa na maskini fimbo hiyo mkononi mwake akiitikisa-tikisa.

74 Sasa, fimbo kavu ikienda kukabiliana na jeshi kubwa la Misri, ambalo lilikuwa limeushinda ulimwengu katika siku zake, maelfu mara maelfu ya magari, wapanda farasi, warusha mikuki, majeshi makubwa mno yaliyotumia mashine; kama vile mtu mmoja angejaribu kukabiliana na Urusi siku hizi ama kitu kama hicho, labda angekabiliwa na mikasa mikubwa zaidi wakati huo.

75 Naye Musa, mwenye umri wa miaka themanini, ninawazia ana upara juu, na masharubu yakining'inia chini, na nywele shingoni mwake, na—na huyo hapo akimwongoza nyumbu huyu, akishuka kwenda kuiteka. Na sehemu yake nzuri, aliiteka (Hiyo ni kweli.), kwa sababu Mungu alikuwa ametoa ahadi.

76 Mungu anapoahidi chochote, Mungu anawajibika kutimiza ahadi Yake. Mungu sikuzote ataitetea. Sijali yale Mu-. . . kile mtu yeyote asemacho juu yake, Mungu anaposema ni hivyo, ni hivyo. Itulize nafsi yako, mwili, na nguvu juu yake, kwa maana Mungu anawajibika kwa Neno Lake. Amina. Ninashukuru sana kwa wimbo huo mdogo tunaoimba:

> Kila ahadi katika kile Kitabu ni yangu,
> Kila mlango, kila kifungu, kila mstari.
> Ninatumainia upendo Wake wa Kiungu,
> Kila ahadi katika kile Kitabu ni yangu.

77 Ni kwa yeyote atakaye, na aje ainywee hiyo chemchemi ya Maji ya Bwana, bure, bila pesa, bila gharama; imelipiwa tayari. Mtu yeyote anaweza kuja na kunywa.

78 Musa akishuka kwenda kuiteka; hiyo ilikuwa tamasha ya jinsi gani. Ndipo alipofika kule chini, alichukua maskini fimbo, ndiyo kitu pekee alichokuwa nacho mkononi mwake, ndipo akaiteka Misri, na akawaongoza wana wa Israeli, na kuwalisha kwa fimbo ile ile mpaka wakaenda kwenye nchi ya ahadi. Amina. Maskini fimbo kavu! Huenda usiwe na mengi sana mkononi

mwako. Huenda hata usiweze kupiga mbinja. Lakini chochote ulicho nacho mkononi mwako, mwachie Mungu akishike Naye atakibariki. Amina.

79 Ikiwa huwezi kufanya zaidi ya kumshuhudia jirani yako, kama huwezi kufanya zaidi ya kuinua mkono wako, useme, "Mungu, ninakubali kila Neno Lake," chukua kilicho mkononi mwako na ufanye uwezavyo kwa utukufu wa Mungu.

80 Kulikuwa na mvulana mdogo, wakati mmoja, alikwenda kumwona Yesu, naye alikuwa na biskuti ndogo nne ama tano na samaki mle ndani. Sasa, katika mkono wa huyo mvulana mdogo hakikufaa sana, lakini mara kikiwa mikononi mwa Bwana Yesu Kristo, alikibariki na kuwalisha elfu tano. Kitu kidogo ulicho nacho kinaweza kuwa ni cheche ndogo ya imani iliyo hapo chini, kwamba unaamini kwamba alifufuka katika wafu. Haifai sana kwako, lakini ifungulie wakati mmoja katika ushuhuda, inaweza kuwa ndiyo sababu ya mamia ya watu kumjia Bwana Yesu Kristo.

81 Kama umeketi hapo mgonjwa au kilema, nawe una chembe ndogo ya imani, iachilie usiku wa leo na useme, "Bwana Yesu, hii ndiyo tu niliyo nayo, kulitumainia Neno Lako, nami huyu hapa naja, ni juu Yako kuyashughulikia mengine yote." Mungu atakwambia mengine yote pia. Wewe iachilie tu na umruhusu Yeye aichukue.

82 Yesu aliachilia atomi ya aina gani basi? Alichukua samaki, hakuwalisha tu kwa samaki wabichi au samaki walio hai, aliwalisha samaki waliopikwa na mkate uliookwa. Amina. Alipoipata sijui. Hata hivyo, Yeye—Yeye aliwalisha nao wakala.

Kama vile jamaa mmoja alivyosema, si muda mrefu uliopita, alisema, "Kwani unaamini hadithi hiyo kuhusu Eliya kuketi kule juu pamoja na kunguru?"

Nikasema, "Naam, bwana. Ninaamini kila neno lake." Hiyo ni kweli.

83 Walidhania Eliya alikuwa mwendawazimu, akiwa ameketi juu ya mlima kule, naye alikuwa akinywa maji kila alipotaka. Nayo ile jamii na watu wa tabaka la juu kule chini walikuwa wakifa kwa njaa, halafu wakamwita mwendawazimu. Naye alikuwa na hali bora kuliko watu wengi, alikuwa na watumishi weusi ambao walimbebea chakula kila alipokuwa na njaa. Hiyo ni bora zaidi kuliko watu wengi wanaoketi hapa usiku wa leo. Hiyo ni kweli. Kila wakati aliposhikwa na njaa, huyu hapa kunguru anakuja na sambusa na kumpa, akaruka akaondoka. Alipiga magoti akanywa maji alipotaka. Alikuwa katika mapenzi ya Mungu. Aliliamini Neno la Mungu. Amina. Hilo—hilo—hilo tu ndilo unalopaswa kufanya, ni kuamini Neno Lake.

Mtu fulani alisema, "Sasa, Ndugu Branham unamaanisha kweli kwamba kunguru huyo alimletea sambusa?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Vema, huyo kunguru aliipata wapi?"

84 Nikasema, "Sijui. Kunguru aliichukua na kumletea Eliya, naye akala." Nikasema, "Hivyo ndivyo ilivyo kwa Roho Mtakatifu. Ulikuwa ukinidhihaki nikipaza sauti." Nikasema, "Siwezi kukwambia ilikotoka; Roho Mtakatifu huileta. Ninaila tu. Na ninaipenda na ninaishi kwayo. sijui inatoka wapi; lakini naipata; hilo ndilo jambo pekee ninalojua. Maadamu Yeye anaileta, niko tayari kuichukua." Amina.

85 Aisee, "Huyo jamaa atatembeaje huku haendi kwa daktari?" Siwezi kusaidia hilo; Mungu anaposema hivyo, atafanya kwa vyovyote vile. Wewe tazama tu. Ni wajibu wa Mungu kulishughulikia Neno Lake. Yeye huliangalia apate kulitimiza, na Yeye anawajibika Kwake. Naye atafanya hivyo katika kila jambo (Amina.) kwa mwanamume yeyote au mwanamke atakayethubutu kuliamini Neno Lake (Loo, jamani, hiyo ni kweli, naam, bwana. Musa alishuka akaenda kule, naye akafanya vile hasa Bwana alivyomwambia afanye.), ukichukua tu kile ulicho nacho mkononi mwako na kumwachia Mungu.

86 Sasa, kulikuwa na jamaa mdogo wakati mmoja, baadaye kidogo kutoka pale, jina la—lake Daudi, maskini mvulana mdogo mchungaji aliyeishi mlimani, akiwalisha kondoo wa baba yake. Lakini alijua baraka za Bwana zilikuwa juu yake. Kwa hiyo alijua ya kwamba Mungu alikuwa pamoja naye. Basi siku moja wakati majeshi ya Israeli yalipokuwa yamekusanyika kupigana na Wafilisti, mbona, Yese baba yake alisema, "Sasa, nitakutuma kwa ndugu zako; wapelekee zabibu na kadhalika, ndipo uende ukaone jinsi ndugu zako wanavyoendelea." Wavulana wawili wakubwa walikuwa vitani.

87 Basi Daudi akatoka. Nanyi mnajua alipofika kule, aliona tamasha. Wafilisti walikusanyika upande mmoja na Israeli upande mwingine. Sauli ameketi pale, urefu wa futi saba, inchi nne ama *chochote kile,* jamaa mkubwa mno anayeonekana wa kifalme. Lakini ng'ambo, ng'ambo ya lile bonde, ng'ambo ile kulikuwa na jeshi la Wafilisti, nao walikuwa na mpinzani mkuu, ama, bingwa mkubwa jina lake Goliathi. Jamani, alikuwa yapata urefu wa futi tisa na inchi nne, naye alikuwa mtu wa jinsi gani. Naye ibilisi anapojua kwamba amekushinda kidogo, basi hakika atajigamba kwako, kama akiweza.

88 Basi akatoka ubavuni mwa kilima huko, akasema, "Nitawapa pendekezo, ninyi jamaa wote. Hebu tusisababishe umwagikaji wowote wa damu." Mnaona? Yeye ni mkubwa, naye alikuwa amewashinda wote. Hivyo akasema, "Ninyi tumeni . . . ninyi jichagulieni mtu huko katika majeshi ya Israeli, na aje huku, na kupigana nami; ndipo nikimwua, basi ninyi nyote mnatutumikia sisi, akiniua, basi tutawatumikia ninyi." Hakika. Hivyo ndivyo ibilisi atakavyofanya.

Sasa, hebu chukua kwa mfano jamaa huyu hapa: "Laiti ningeliona *huyu*, ama *yule*, ama *yule*." Mnaona? Wakati wowote wanapoweza kupata wazo la namna hiyo . . .

89 Lakini siku moja alifanya majivuno kwenye sikio la mtu mwingine. Kulikuwa na maskini jamaa aliyeonekana mkondefu, pengine alikuwa na uzito wa takriban pauni mia moja na kumi, huku mabega kidogo yameinama huku amejifunga kanzu ndogo ya mchungaji. Basi asubuhi hiyo, huku majeshi yakienda huku na huko, na kupigiana makelele, na kujaribu kuingia kwenye vita, mbona, mpinzani huyu mkubwa alijitokeza, akasema, "Sasa, ninayatukana majeshi ya Israeli." Lakini yaliangukia masikio ya mtu mwingine kwake basi. Naam, bwana.

90 Kulikuwako na maskini mvulana mdogo pale ambaye alijua alichokuwa anazungumzia. Alisema, "Ni nini hii? Mnataka kuniambia mtasimama na kuruhusu . . . Mfilisti huyo asiyetahiriwa kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai?" Amina. Alijua alichokuwa anazungumzia. Loo, jamani. Goliathi, ulijisifu vibaya basi.

91 Ndipo hilo lilipoliangukia sikio la Daudi, basi nduguye akasema, "Sasa, angalia hapa, ninajua utundu wa moyo wako, sasa, achana tu na kusema mambo kama hayo."

92 Baadhi yao wakasema, "Mbona, anaweza kumwoa binti wa mfalme, naye atampa mali, nayo nyumba ya baba yake itakuwa huru katika Israeli, na kadhalika."

Akasema, "Haya yote mnayozungumzia ni ya nini sasa?" Jamani, jamaa mdogo tu, hivyo ndivyo tu yeye . . .

93 Mbona, huwezi kuitegemea sura. Hiyo ni kweli. Hutegemei sura. Unaenda na kilicho moyoni. Hiyo ni kweli. Ukienda kwa sura, mbona, Israeli wangelikuwa na wakati mgumu sana walipodhania wangeweza kupata maji kutoka kwenye mwamba. Hapo ndipo mahali pakavu zaidi palipokuwako nchini. Lakini Mungu alisema "Nena na mwamba. Hicho ndicho kitu kilicho na maji."

94 Ndipo wanasema siku hizi, "Ikiwa kuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, ungekuwa katika baadhi ya makanisa hayo makubwa makubwa ya kale." Hayo ndiyo tu unayowazia. Unaona? Hiyo ni kweli. Labda ndipo mahali pakavu sana ulipowahi kuona, lakini kuna maji pale kama utanena nayo tu. Amina.

95 Sasa, nawatakeni muone. Ndipo wakati Daudi, ninaweza tu kumwona akienda kule, naye akasema . . . wakamleta mbele ya mfalme. Kasema, "Sasa, ngoja kidogo hapa," kasema, "mpandishe huyo kijana hapa juu." Akamwendea, siku hiyo . . . Sauli alimwita "barobaro." Hapana shaka alikuwa maskini jamaa aliyekonda (Mnajua?), mabega madogo yaliyosinyaa, kidogo akitembea, huku amekodolewa maskini macho

maangavu. Akasema, "Vema, sikiliza, huwezi kupigana na huyo."

96 Akasema, "Moyo wa mtu yeyote usizimie ndani yake kwa sababu ya jitu hili." Kasema, "Mtumishi wako ataenda kule na kupigana naye." Loo, jamani. Napenda ujasiri huo. Nanyi je? Kwa nini? Tutaona katika dakika moja kwa nini alikuwa na ujasiri huo, ni nini kilileta tofauti hiyo. Naam, bwana. Akasema, "Nitaenda kule na kupigana na jitu hilo."

97 Na hapo, Sauli, yule mtoto mchanga mkubwa, ameketi pale juu, karibu sana kutoshana na jitu, na anadhaniwa kuwa mfalme katika Israeli, na *haya* yote, halafu ameketi pale akiogopa kwenda kupigana naye.

98 Inanikumbusha wengi wa watu hawa leo, ambao hawaamini katika uponyaji wa Kiungu. Wanadai kuiamini Biblia, na halafu watamwacha tu ibilisi awakanyagie chini, chochote kile. Ninaamini katika ujuzi wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu, wa kuzaliwa mara ya pili, wenye shina, uliokufa maradufu. Ni—ninaamini katika kitu kinachomfanya mtu kuwa hai. Kinamtia ujasiri na Moto. Hiyo ni kweli. Itamfanya asimame ana kwa ana na ibilisi juu ya ahadi yoyote ya Kiungu ya Mungu na kuiita kweli, haijalishi inaonekanaje. Maskini kijana Daudi . . .

Mbona, alisema, "Huwezi kufanya hivyo."

Akasema, "Wewe acha niende."

Akasema, "Sasa, unajuaje kwamba unaweza kufanya hivyo?"

99 Akasema, "Angalia hapa. Nitakwambia jambo fulani. Nimekuwa na ujuzi fulani." Huo ndio unaohitajika siku hizi, ni mtu ambaye amekuwa na ujuzi.

100 Daudi akasema, "Nimepata ujuzi." Kasema, "Nilikuwa nikichunga kondoo wa baba yangu huko nje, ndipo simba akaingia, dubu akaingia, na kumkamata mwana-mbuzi, ama, mwana-kondoo mdogo, na kukimbia naye," kisha kasema, "Nilimfuatilia na kumpiga kichwani kwa kombeo, ndipo nilipoanza kumpokonya huyo mwana-kondoo kinywani mwake, akainuka, nami nikamwua." Akasema, "Mungu aliyemtia huyo simba mikononi mwangu, na dubu mikononi mwangu," akasema, "ni zaidi sana vipi atakavyomtia huyo Mfilisti asiyetahiriwa." Hiyo ni kweli.

101 Basi Sauli akasema, "Njoo hapa nami nitakufanya mhubiri halisi wa kikanisa, basi." Kwa hiyo anampeleka kule, naye anamvalisha vazi kubwa la vita, na helmeti yake, na kila kitu. Akaivuta chini ya masikio yake madogo, na hebu wazia akichungulia nje pembeni, huku amevaa silaha kubwa mno, wala asingeweza kusogea. Kamwe asingeweza kwenda mbele.

102 Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Mtu anapopata wito mdogo moyoni mwake kwenda kuhubiri Injili, inakubidi

kumpeleka kwenye mojawapo ya hizi seminari kubwa, ama chochote kile kule, na kumpiga na kumwondoshea mhubiri wote, na kuingiza baadhi ya theolojia hii ya kilimwengu ndani yake, namna *hiyo*, na kumwondolea mhubiri wote aliye ndani yake, kisha umwambie aende. Si ajabu hawezi kuamini. Jamani, amefungwa nira kabisa na ulimwengu. Haleluya!

103 Tunapaswa kutoka na kumtikisia baadhi ya Roho Mtakatifu wa mtindo wa kale na kuziyeyusha kabisa nyumba hizi za maiti, tunachohitaji hapa, ni huyo. Amina. Naam, bwana.

104 Maskini Daudi hapo, akavaa ninii zake . . . alikuwa na digrii yake ya B.A., mwajua, na L.L. ya—yake, na L. maradufu D., na D.D., mwajua, amevaa zote. Alisema, "Sijui chochote kuhusu mambo haya. Sikuwahi kuthibitisha chochote. Sijui hizo ni nini." Kasema, "Siwezi kufanya hivyo." Naye Sauli akagundua upesi sana, ya kwamba vazi lake la kikanisa halikumwenea mtu wa Mungu. Amina.

105 Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Ukivua tu maskini mavazi hayo ya kikanisa na kuinama . . . Afadhali niwe na ujuzi wa kale . . . Ni afadhali kijana wangu angekutana na mtu ambaye hajui ABC zake, na kumpeleka hapa nje ubavuni mwa kilima karibu na kisiki cha kale mahali fulani, na kumwombea sana apate ujuzi wa kale wa Roho Mtakatifu, kuliko kumpeleka shule zote zilizoko nchini, ambazo zingeondoa nguvu za Mungu na baraka za Mungu maishani mwake. Amina. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

106 Na hapo, Daudi akakiangalia kitu hicho, akasema, "Sijui lolote kuhusu hiki. Sijui jinsi ya kusema, 'Ah-mina,' na doksolojia zote, na mambo hayo yote namna hiyo. Sijui mnavyofanya hivyo." Kasema, "Acheni niende na kile ambacho tayari nimethibitisha kuwa ni cha kweli." Haleluya!

107 Hivyo ndivyo ninavyosema. Ninajua nilipoenda kwa mwangalizi wangu mkuu, nikamwambia Malaika wa Bwana alikuwa amekutana nami, akasema, "Billy, nenda nyumbani. Ulikuwa na jinamizi." Akasema, "Mbona, unamaanisha ukiwa na elimu ya darasa la saba, utawaombea wagonjwa, kisha uende ukawaombee wafalme?"

Nikasema, "Hivyo ndivyo alivyosema."

Kasema, "Utafanyaje hilo?"

Nikasema, "Sijui, lakini limenifikisha umbali huu, Yeye ataniongoza." Mungu anaweza, Yeye aliyeitoa hiyo ahadi, ataitimiza.

108 Akasema, "Aa, mwanangu, naona afadhali urudi. Unahitaji kupumzika." Sikuhitaji kupumzika. Nilihitaji kwenda kazini. Nilikuwa nimepumzika kwa muda mrefu sana wakati huo.

109 Hiyo ndiyo shida ya watu wengi sana siku hizi. Amka uingie kazini. Wakati umefika, watu wana shida, hima twendeni, tuwapeleke kwa Bwana Yesu, haraka.

110 Tunaona hapo kwamba tunamwona maskini Daudi, alisema, "Sasa, tazama. Sijui chochote kuhusu ninii yako . . . digrii zako zote, wala sijui chochote kuhusu silaha zako, na vitu vyote ambavyo ninyi jamaa mnapigana kwavyo, na kugombania, na kuzozania. Lakini najua jambo moja: nimeliamini maskini kombeo hili la kale; Mungu alimpiga yule simba kwa kombeo hili; alivipiga vitu hivi vingine vyote kwa kombeo hili; naye Mungu atampiga huyo Mfilisti asiyetahiriwa kwa kombeo."

111 Ninajua ya kwamba nilipokuwa mwenye dhambi, nimepotea, na katika ulimwengu, nikifa bila Kristo, Roho Mtakatifu aliniokoa. Ninajua ninapochoka, Roho Mtakatifu hunichangamsha. Ninajua ninapohitaji chakula, Roho Mtakatifu hunilisha. Ni zaidi sana vipi Roho Mtakatifu ataniponya kama mimi ni mgonjwa, baada ya Mungu kuahidi jambo hilo. Sijui kuhusu mambo yako mengine, lakini najua Mungu ametoa ahadi, na ni ahadi ya Mungu, na Mungu atadumu na ahadi Yake.

"Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako Daudi?"

Akasema, "Kombeo." Amina.

"Utapiganaje na lile jitu huko nje lenye mkuki wa futi kumi na tano ama ishirini? Usingeweza kumkaribia."

Akasema, "Nililithibitisha hili. Najua kile hili litafanya."

112 Hiyo ni kweli. Loo, mwanamume ama mwanamke akipata kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, aliyewahi kumpokea Roho Mtakatifu, wanajua hilo litafanya nini. Sijui yale mabishano yenu yote na shule zenu zote zitakayofundisha, ila ninajua jambo moja, ya kwamba litafanya yale Mungu aliyosema lingefanya.

113 Maskini Daudi alikuwa amemjua Mungu kwa njia ya maumbile. Akiwa huko nje, akiendelea, alizungumza juu ya maji matulivu na majani mabichi. Alimwona Mungu katika hali Yake ya kale, Mungu katika maumbile Yake, akitenda kazi.

114 Mungu yuko katika maumbile. Je, huamini hilo? Hakika Yeye yuko. Ninapenda tu kumwangalia katika machweo ya jua, kumwangalia katika . . . katika kukua kwa maua, kumwangalia wakati jua likichomoza.

115 Hapa siku moja, nilikuwa juu milimani ninakoenda ninapochoka sana hata siwezi kwenda mbele zaidi. Nami nilienda kule kwenye majira ya majani kupukutika kuwinda, nami nilikuwa nikiwinda kulungu. Ilikuwa karibu mwisho wa majira ya kupukutika. Tulikuwa huko nyuma kabisa, kwa sababu theluji ilikuwa haijashuka kulisukuma hilo kundi chini. Nami nilikuwa juu sana, ama, karibu na mpaka wa msitu. Na mwishoni mwa mwaka, huko juu kabisa kwenye milima mirefu,

inakuja, theluji itaanguka kidogo, kisha mvua inyeshe kidogo, na kisha jua linachomoza, mnajua jinsi inavyokuwa mwishoni mwa mwaka. Basi nilipokuwa nikienda mbele, si kuwapiga wanyama risasi, si lingine ila nipate kuwa mbali peke yangu.

116 Ninapenda kwenda mbali pamoja na Mungu. Kila mwanamume na mwanamke. . .Hiyo ndiyo shida. Unapaswa kutumia muda mwingi kila siku, badala ya kuzunguka-zunguka, na kukimbia huku na huko, unapaswa kuwa huko nje mahali fulani ukiomba na kumtafuta Mungu. Amina.

117 Na huko juu, nilikuwa nikitembea; ndipo dhoruba ikatokea, nami nikaingia nyuma ya mti namna *hii*. Nami nilikuwa nimesimama nyuma ya mti huku pepo zikivuma. Palikuwa ni mahali wazi pale hata hivyo. Kwa hiyo basi, baada ya dhoruba kwisha, nilitoka nyuma ya ule mti, nilikuwa nimeilaza bunduki yangu chini. Nami nikatazama, ndipo nikaanza kusikia kundi la kulungu mbali sana mbele yangu. Walipotea katika dhoruba. Walikuwa wakiitana.

118 Mama yangu ni nusu Mhindi, na hiyo, ya kutosha tu kwamba ninapenda tu huko porini. Loo, jamani. Kama Daudi alivyosema, “Kilindi kinapoanza kuita kilindi. . . ” Na kwa kweli kilianza kuita kilindi basi.

119 Maskini mbwa mwitu wa kijivu akaanza kulia hapa, naye mwenzake akamjibu huko chini kabisa. Nililia kama mtoto mchanga. Nisingeweza kujizuia, nilisimama tu pale na kuguta huku nikiwa nimeinua mikono yangu hewani.

120 Nikatazama huko nje; ndipo jua likachomoza, huko nyuma kabisa kwenye upeo wa macho wa magharibi, likipenyeza, jicho lile kubwa lionalo kote. Na juu. . .hiyo miti isiyokauka majani ilikuwa imeganda, kule juu, kwa barafu. Ilifanya upinde wa mvua chini kuvuka bonde namna *hiyo*. Nikawazia, “Ee Mungu, kila mahali unapotazama unaweza kumwona.” Huyo hapo. Nilidhani Yeye. . .Huyo hapo akiangalia kule; anachungulia kote. Huyo hapo katika hilo kundi la kulungu, na huyu hapa huko chini katika mbwa-mwitu wakipiga kelele. Huyu hapa katika maumbile. Nikawazia, “Ni. . . ” (kama Petro alivyosema) “Ni vizuri sisi kuwapo hapa. Na tujenge vibanda vitatu.”

121 Nami nikasikia kubarikiwa sana, ndipo nikazunguka mti huo mbio tena na tena, nikipiga mayowe kwa sauti yangu yote, nikipiga tu mayowe na kuruka-ruka kwa nguvu nilivyoweza. Kama mtu angalikuja huko, wangetaka kunipeleka kwenye taasisi ya wendawazimu, wakifikiri kuna mwendawazimu huko msituni. Lakini nilikuwa yapata maili thelathini na tano au arobaini kutoka kwenye ustaarabu. Nilikuwa peke yangu na Bwana, nikiwa na wakati mzuri.

122 Nikatazama juu, nikauona huo, nikawaza, “Naam, upinde ule wa mvua.” Mungu alimpa huo Nuhu. “Alionekana mithili ya upinde wa mvua kama jiwe la yaspi na akiki. Wa kwanza,

wa mwisho, Yeye aliyekuwepo, aliyeko, na atakayekuja, Shina na Mzao wa Daudi, ile Nyota ya Asubuhi." Nami nikazunguka na kuzunguka mti huo tena, kwa nguvu tu nilivyoweza kwenda, nikipiga makelele tu kwa sauti yangu yote.

123 Ndipo kuchakulo mdogo wa misonobari, sijui kama ninyi ndugu mmewahi kumwona mmoja ama la, lakini maskini kuchakulo wa misonobari alikuwa ameketi pale juu ya kisiki. Akaanza, "Kwe, kwe, kwe, kwe, kwe, kwe, kwe," kana kwamba atanirarua vipande vipande. Nikawazia, "Maskini huyu jamaa mdogo anasisimkwa na nini?" Alikuwa akipayuka payuka tu hivyo.

124 Nami nikatazama kule, nikawaza, "Labda ananiogopa." Na hivyo basi ikatokea niliangalia na kutoka chini pale, upepo ulikuwa—ulikuwa umemwangusha chini tai mkubwa. Naye tai huyo mkubwa, alipojitokeza, huyo ndiye maskini yule kuchakulo alikuwa akimbwekea. Aliruka juu ya tawi namna *hiyo*, naye maskini yule kuchakulo akaruka nyuma katika kupayuka-payuka kwake.

125 Nilimtazama tai huyo mkubwa. Nikawaza, "Sasa, Bwana, hivi nilimtisha yule tai akatoka huko, nilikuwa nikipaza sauti sana?" Kwa hivyo nilimtazama na kuwazia, "Sasa, Wewe umemweka hapa mbele yangu, nione, jambo fulani. Sijui ni kwa nini ulimleta tai huyo mbele yangu."

126 Niliendelea kumtazama. Loo, alikuwa ndege mkubwa, mkubwa mno. Nami niliona macho yake makubwa ya mahameli yakitazama huku na huko. Nikawazia, "Vema, kuna jambo moja ninalokupendea, jamani: hilo ni, wewe ni jasiri, huogopi." Kisha nikawazia, "Kwa nini huna hofu? Hilo ndilo ninalotaka kujua. Kwa nini huogopi? Hivi huniogopi?" Nami nikamtazama, mwajua, naye angeyakung'uta hayo manyoya huku na huko, mwajua, na kutembea huku na huko kwenye gogo hilo, akitazama pande zote. Akamwangalia kuchakulo huyo wa misonobari kisha akaniangalia. Nikasema, "Jamani, unajua ningeweza kukupiga risasi?" Akaniangalia tu na kuendelea, mwajua, akikanyaga kwa kishindo huku na huku. Hakuwa akisumbuka sana.

127 Nami nikawazia, "Kwa nini hu—huogopi?" Kisha nikatokea kusema, "Sasa, nitasoma, Bwana, kwa nini? Sasa, ninakuona pale kwenye upinde wa mvua; nilikuwa nikisikia kundi la mbwa mwitu; ninakuona huko katika machweo ya jua. Mbona? Je, Wewe uko katika tai yule?" Nami nikamwangalia yule jamaa kidogo. Nikawazia, "Naam, sababu ya yeye kutoogopa, a—anayasogeza manyoya hayo huku na huku. Mungu alimpa jozi ya mbawa, naye anajua ya kwamba kabla sijaishika hiyo bunduki mkononi mwangu, angekuwa kwenye vile vilele vya miti, wala nisingeweza kumpiga risasi." Nikasema, "Utukufu kwa Mungu." Nikawa na kipindi kingine. Mimi huyu hapa

nikaanza kukimbia. Nikawazia, "Hiyo ni kweli. Mradi unaweza kumhisi Roho Mtakatifu karibu nawe, yanayotokea yanaleta tofauti gani? Achilia kila kitu, chochote kiwezacho. Maadamu unaweza kumhisi karibu nawe, jua Yeye yuko hapa."

Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, hivi huogopi kwamba utafanya kosa usiku mmoja?"

Nikasema, "Hapana, si maadamu ninaweza kumhisi Yeye, hapana, bwana, atakapoondoka, nitaondoka jukwaani, lakini maadamu Yeye yuko pale."

128 Nikamtazama jamaa huyo kwa dakika chache. Ninatoka tu kwenye somo langu hapa, lakini nataka kuwaambia hili. Nilipomtazama pale kidogo, baada ya muda kidogo alichoka kumsikiliza maskini kuchakulo yule wa misonobari, "Kwe, kwe, kwe, kwe." Ndipo akafanya tu mruko mmoja mkubwa mno namna *hiyo*; alikuwa moja kwa moja juu ya hivyo vilele vya miti, mapigo kadhaa kwa mabawa yake. Naye kamwe hakupiga mbawa zake mara nyingine, alijua tu jinsi ya kuweka mbawa zake. Nami nikamwangalia. Kila wakati upepo ungeingia, angepanda juu. Kila wakati upepo ungeingia, angepanda juu. Akazidi tu kwenda na kwenda na kwenda na kwenda, mpaka akawa chembe ndogo.

129 Nilisimama pale na kupiga kelele kwa sauti yangu yote. Nikasema, "Naam, Bwana, ndivyo hivyo; ndivyo hivyo. Si kuruka na kujiunga na Methodisti, halafu kurudi kwa Baptisti, kisha kuelekea kwa Presbiteri, kuliendea la Pentekoste, Assemblies, Umoja, kote kote namna hiyo. Ni kutandaza tu mbawa zako." Haleluya! Hiyo ni kweli.

130 Si kukimbia kutoka kwa mkutano mmoja wa uponyaji hadi mwingine. Si kukimbia kutoka ofisi moja ya daktari hadi nyingine. Ni kujua jinsi ya kutandaza mbawa zako za imani katika nguvu za Roho Mtakatifu; kila wakati anapoingia, panda juu Yake mpaka unapoweza kuachana na hizi kwe, kwe, kwe, za duniani. Maskini kundi hili la kale linalosema, "Siku za miujiza zimepita," na, "Hilo lilikuwa la watu wa kale": panda juu yake. Kila wakati Roho Mtakatifu anapoingia ndani, shikiza mbawa zako ndani Yake na utoweke, uendelee mpaka mbingu za Mbingu. Mwache maskini huyo *nanii* wa duniani, anayeketi hapa nyuma na kusema, "Vema, ninaamini siku za miujiza zimepita. Ninaamini kuwa watu hao wanaowazia hivyo wamerukwa tu na akili." Panda tu juu yake. Amina. Usipigepige mbawa na kuruka, weka tu mbawa zako. Acha Roho Mtakatifu akunyakue, akunyakue, akunyakue. Endelea mbele tu, hadi utoweke.

131 Naam, siku moja kule juu nilikuwa nikichunga ng'ombe. Ilitokea sikuona kitu kuhusu ta-. . ., au, jambo lingine kuhusu tai: Maskini mama tai anapotengeneza kiota chake, hukitengeneza kwa vijiti vikubwa na kadhalika, nacho kinavunda kandokando.

132 Kwa hivyo tai wadogo wanapojifunza kuruka, nilikuwa nikiona, nikashikiza, nikafungia hatamu za farasi wangu kwenye tawi, nikaenda kule. Nilikuwa na darubini nikitazama tu. Nikamwona yule mama tai mzee huko juu kabisa; alikuwa akifanya jambo fulani, akipigapiga mbawa hewani. Nikamlenga kwa darubini yangu na kumwangalia, maana tulikuwa tunawashusha ng'ombe. Ndipo nikatazama mle ndani, nikamwona, jinsi alivyokuwa akiwatoa nje hao vifaranga. Naye akaendelea kuwasukuma-sukuma huku na huko hao vifaranga wa tai huko juu.

133 Ndipo baada ya kitambo kidogo, akawabeba wote kwa mbawa zake; naye akawatoa tu kutoka kwenye kiota hicho kinachovunda, akashuka bondeni, naye akatandaza mbawa zake kubwa chini namna *hiyo*, basi alipofanya hivyo, hao vifaranga wote wa tai wakashuka na kuanza kutembea-tembea huku na huku. Mara ya kwanza walipowahi kukanyaga nyasi, jamani, kama hawakuwa na wakati mzuri. Nikasema, "Bwana, kama huo si uamsho wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu, sijawahi kuona mmoja maishani mwangu." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Watazame!"

134 Kutoka kwenye maskini kiota hicho kinachovunda huko juu, mwajua, ambapo maskini ile harufu ya kale na vichomi na kadhalika, hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Anakuinua juu kwenye mbawa za tai, na kukutoa katika mambo ya kale yanayovunda ya ulimwengu akakwingiza mahali hapa ambapo mambo yote yanawezekana, huru uwezavyo kuwa. Amina.

135 Kisha nikawaona wakikimbia huku na huku, wakinyakua funda la nyasi *hapa*, na kukimbia kule, kunyakua funda *hapa*, na kucheza, wakiwa tu na wakati mzuri sana, bila lawama hata kidogo. Nikawazia, "Vema sasa, maskini mama huyo atafanya nini?"

136 Baada ya kuona vifaranga wake wakianza kucheza vizuri sana na kuwa na wakati mzuri, aliyatandaza mabawa yake tena, naye akapanda moja kwa moja hadi kwenye mwamba wa juu kabisa ambao angeweza kupata. Akaketi pale na kutulia, akaanza kutazama pande zote. Loo, jamani. Nikawazia, "Hiyo ni kweli. Wakati Bwana Yesu aliponitoa katika udongo wa matope na kuniweka juu ya Mwamba, Kristo Yesu, alipanda ngome za Utukufu, akiketi huko juu, akitazama chini. Jicho Lake liko juu ya shomoro, na ninajua Yeye ananitazama." Hakuna madhara, hakuna hatari, hakuna kitu kingine chochote kinachoweza kutukia, maadamu tuko katika Uwepo Wake wa Kiungu. Amina. Liwe liwalo; hata mauti yenyewe imepoteza uchungu wake. Maana amesimama kule Utukufuni usiku wa leo; macho Yake yanautazama mkutano huu kuona ni nini hasa kitakachotukia, wakati watoto wake wadogo wanakusanyika pamoja kukizunguka kiti cha enzi cha Mungu, wakishangilia

katika Neno la Mungu, wakipiga makelele katika Uwepo wa Mungu, loo, jamani, bila wasiwasi.

137 Hao jamaa wadogo hawakuangalia chochote. Jamani, hebu mbwa mwitu aelekee kwa mmoja wao, angecharazwa viboko vibaya sana alivyopata kucharazwa maishani mwake. Amina. Loo, jamani.

138 Ndipo alipoketi pale, basi baada ya kitambo kidogo, niliketi pale yapata saa mbili nikimtazama. Maskini dhoruba ndogo ya kaskazini ikatokea, mchirizi mdogo wa kijani kibichi, ukaja mbio, dhoruba inakuja. Ndipo wakati alipopiga yowe, alipoondoka kwenye kiota kile kule juu, aliruka chini namna *hiyo*, akapiga yowe moja, ndipo hao vifaranga wote wa tai kote kwenye hilo konde do—dogo pale wakakimbia pamoja. Akarusha mbawa zake namna *hiyo*. Kila mmoja wa hao vifaranga akakimbia tu na kuruka juu ya bawa, wakaweka mdomo wao mdogo kwenye unyoya namna *hiyo*. Akainua mbawa hizo kubwa mno, huku dhoruba hiyo ikishuka kwenye kilima hicho ikipiga kelele maili sitini kwa saa. Akaenda moja kwa moja kwenye mwamba kadiri alivyoweza na kuwapeleka kwenye kimbilio.

139 Nikawazia, "Naam, baadhi ya siku hizi, kutakuja sauti kutoka juu; Bwana Yesu atakuja na kunyoosha mbawa Zake kubwa, ndipo watoto Wake wote wadogo wataruka mikononi mwa msalaba wa kale uliochakaa, nasi tutabebwa tuingizwe kwenye usalama wa siku Yake ijayo mpaka dhoruba ya maisha itakapokwisha." Loo, ni ajabu jinsi gani endapo utamtazama Mungu, juu ya asili Yake.

140 Daudi alikuwa ameona hili na alijua ya kwamba Mungu alikuwako, na Mungu angekomboa. Alikuwa amemwona Mungu katika maumbile Yake. Kwa hiyo akasema, "Nipe kombeo hili dogo. Nimelijaribu. Hicho ndicho kitu pekee ninachojua lolote kukihusu, ni kombeo hili."

141 Na hayo tu ndiyo mwaminio anayojua lolote kuhusu, "Kwamba Mungu alisema hivyo, na hili ndilo kombeo la kale. Nitalitumaini wakati wowote, dhidi ya chochote ambacho ibilisi anaweza kutoa," (Amina!) "ni Neno la Mungu."

Neno la Mungu pekee litamshinda Shetani mahali popote, wakati wowote, kwenye hali zozote, kama mwanamume ama mwanamke atathubutu kumwamini, Mungu, kwenye Neno Lake. Amina.

Basi ninaweza kumwona basi, kama alivyosema, "Vema, endelea. Bwana awe pamoja nawe."

142 Akashuka kule chini na kujitafutia huko katika lile bonde la kale akaokota mawe matano madogo, naye akayaweka kwenye mkoba wake mdogo. Akaingiza moja kwenye kombeo lake akatoka kwenda kukabiliana na Goliathi. Ndipo Goliathi akamwangalia na kusema, "Kwani mimi ni mbwa?" Mbona, akamlaani kwa jina la miungu yake. Alisema, "Nitakunyanyua,

wewe maskini wewe mwenye sura kama cheche, mtakatifu anayejifingirisha, wewe, na kuuchomelea mkuki huu ndani yako, na kukuning'iniza hapa juu na kuwaacha ndege wakule kwa muda kidogo." Naam, bwana.

Unasema, "Daudi hakuwa mtakatifu anayejifingirisha." Naam, alikuwa; mnachokiita mtakatifu anayejifingirisha.

Wakati Sanduku la Bwana lilipoanza kuingia, alitoka na kucheza mbele ya hilo Sanduku kwa nguvu tu alivyoweza; ndipo mkewe akamdhihaki.

143 Kasema, "Usipopenda hiyo, tazama hii." Ndipo akashuka akalizunguka hilo Sanduku tena na tena na tena. Kama huyo si mtakatifu anayejifingirisha wa kisasa, sijapata kumwona mmoja maishani mwangu. Hakika alikuwa. Amina.

Mtu fulani alisema, "Ndugu Branham una baadhi ya namna hizo hapo za dini mpya, sivyo?"

Nikasema, "Hapana, nilipata dozi nzuri ya namna ile ya kale." Amina.

Kasema, "Nikasema, namaanisha hiyo dini ya kupiga makelele."

144 Nikasema, "Hiyo ndiyo dini ya zamani zaidi iliyopata kujulikana." Nikasema, "Mungu alimwuliza Ayubu, 'Ulikuwa wapi nilipoweka misingi ya nchi, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha?' miaka elfu kumi kabla ya ulimwengu kuumbwa." Amina. Mtaniita "mtakatifu anayejifingirisha" kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali mjitayarishe, mlizoee.

145 Angalieni, ndugu, hebu niwaambie jambo fulani. Daudi alijua, naye akakunja maskini kombeo hilo. Akatoka nje, naye akasema, "Wewe unanijia kama Mfilisti, kwa jina la Mfilisti, na dereya na mkuki, lakini mimi ninakujia kwa Jina la Bwana, Mungu wa Israeli wa jeshi lile lile ulilolitukana." Kisha akasema, "Leo nitawapa ndege na wanyama wa kondeni mzoga wako. Nami nitaitwaa mizoga yote ya hawa Wafilisti. . . " Kisha yeye. . . ndipo maskini jamaa yule akaanza kumkaribia.

146 Sasa, mwangalieni Daudi, alipokimbia akavuka kijito hiki kidogo, akavuka kukabiliana naye. Basi alipofanya hivyo, alikuwa na nini mkononi mwake? Hiki hapa alichokuwa nacho Daudi: Alikuwa na mawe matano, I-M-A-N-I, katika vidole vitano vilivyozungushiwa Y-E-S-U [Eng: J-E-S-U-S—Mfa.]; huyu hapa anakuja, mawe matano katika vidole vitano; imani katika Bwana Yesu. Nalo hilo jiwe likaenda moja kwa moja kwenye fuvu la kichwa la maskini jitu hilo, naye Daudi akambwaga chini, kisha akakikata kichwa chake. Naye alipofanya hivyo, alitazama pande zote; ndipo wengine wote wakaona kilichofanyika, wakajipa moyo na kuchomoa

panga zao na kuanza kupigana na Wafilisti hadi ukutani, wakawakatakata.

147 Hapa miaka michache iliyopita, nilipoanza kwa mara ya kwanza, karibu hapakuwa na mtu yeyote aliyehubiri juu ya uponyaji wa Kiungu. Walipomwona Mbunge Upshaw na wengi wao wakiponywa, ninawaambia: Wapresbiteri, na Wamethodisti, na Assemblies of God, na hao wote, walijipatia mmoja; na wengine wakajipatia mmoja; Church of God likajipatia mmoja; Oral Roberts; na hayo mengine yakajipatia mtu mwingine; basi ndugu tumekuwa tukiwakata Wafilisti kutoka kulia kwenda kushoto. Haleluya! Kwa sababu kila moyo unajipa ujasiri usiku wa leo, wala nusu haijapata kusimuliwa bado. Kwa maana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ameahidi.

Je, una nini mkononi mwako usiku wa leo? Chochote ulicho nacho, kitumie kwa utukufu wa Mungu.

148 Ninaweza kumwona jamaa mmoja kule chini jina lake Samsoni. Alitoka huko nje siku moja, nao Wafilisti walikuwa wamefanya madhara kidogo kule; wakafunga mikia ya mbweha wengine, wakateketeza nafaka zao zote. Kwa hiyo Waisraeli hao wakaja na kumkamata, wakasema, “Hatuna budi kukupeleka kwa Wafilisti.”

149 Nao wakampeleka kule, wakamfunga kwa kamba, na kumleta huko chini. Nao Wafilisti walikuwa wanataka kumdhulumu, basi alipofanya hivyo, Roho wa Bwana akaja juu yake. Amina. Hilo ndilo lililoleta tofauti. Alipohisi Roho wa Bwana akimjia, hakuwa na chochote mkononi mwake. Ndipo akatazama chini na hiyo hapo mfupa wa taya ya nyumbu. Basi akauchukua mfupa huo wa taya mkononi mwake na kuwaua Wafilisti elfu moja. Amina. Huo ndio tu aliokuwa nao.

150 Haikumbidi kwenda mbele na kusema, “Sasa, ngojeni. Hebu niupeleke mfupa huu wa taya kule chini nikaupime nione kama utastahimili hilo shinikizo au la.” Hakuwa na muda wa kuyawazia mambo hayo yote. Dharura ilikuwa imeingia. Wafilisti walikuwa wamemvamia. Jambo pekee aliloweza kufanya ni kuokota mfupa wa taya na kupigana. Hakukuwa na lingine.

151 Na usiku wa leo, huna wakati wa kukimbia na kuyawazia mambo haya yote. Uamsho utaisha kesho usiku. Hebu tulichukue Neno la Mungu, lililo mkononi mwenu, tupigane na adui yetu mbaya sana. Amina.

Mungu akampa ushindi.

152 Kulikuwako na maskini jamaa mdogo kule chini katika Biblia, jina lake Shamgari. Huenda hata hukupata kumtambua katika Kitabu cha Waamuzi, jamaa mdogo tu. Hebu tuchukue mchezo mdogo wa kuigiza kwake.

153 Ninaweza kumwona kule, maskini jamaa mdogo. Ilikuwa ni wakati ambapo kila mtu alifanya alivyotaka. Nao Israeli hawakuwa na mfalme. Wote walikuwa wametengana, wamegawanyika, makundi madogo, kama tu kanisa lilivyo leo.

154 Mmoja ni Assemblies. Mwingine ni Church of God. Mwingine ni Umoja. Mwingine ni Mbaptisti. Mwingine ni Mpresbiteri. Mwingine ni Mmethodisti. Loo, jamani. Tusipopapenda *hapa*, tunaenda *hapa*, na *hapa*, na *hapa*, na . . . Loo, jamani. Si—si—sielewi, mimi mwenyewe.

155 Na kisha wanapoingia mle. Na loo, walichohitaji ni . . . kile tu walichohitaji wakati huo, kidogo kilikuwa ni ukombozi wa mtindo wa kale; ndicho tunachohitaji siku hizi (Amina.), kanisa lirudi kwenye imani ya Mungu aliye hai, liirudie ahadi ya Mungu, lirudi kwenye utukufu wa Mungu, lizirudie nguvu za Mungu.

156 Shamgari alikuwa amevikusanya vitu vyake vyote, ngano yake, kama alivyofanya kila mwaka. Na yapata wakati alipokuwa ameyakusanya mazao, ndipo hawa hapa Wafilisti wangekuja na kumpokonya. Hivyo ndivyo tu ibilisi afanyavyo. Karibu tu kile ibilisi anachojua kufanya vizuri. yapata wakati ambapo umejenga ujasiri mdogo, ama chochote kile, ndipo huyu hapa ibilisi anakuja na kukupokonya. Hiyo ni kweli.

157 Kama tu uamsho unaoendelea sasa. Yapata tu wakati unapouanzisha, na utukufu wa Mungu unaanza kushuka, ndipo bingwa tapeli fulani hana budi kuja, na kufanya jambo lisilo sahihi, na kuondoa utukufu kutoka kwenye jambo hilo.

158 Hapa si muda mrefu uliopita, nilishuka, huyu hapa alikuwepo mmoja wa dada zetu Mkristo, aliyejipaka rangi kama Yezebeli. Nikasema, "Kwani kuna nini?"

Akasema, "Naam, utukufu kwa Mungu." Kasema, "Mchungaji wangu aliniambia ni ukombozi wa wanawake."

159 Ati ukombozi wa wanawake! Kwani una shida gani wewe? Hakuna kitu kama hicho. Kristo alikukomboa kutoka dhambini, basi tenda hivyo na uvae hivyo. Yapata wakati kanisa limejengeka na kuanza vizuri, ndipo jambo kama hilo linaingia. Naam, bwana.

160 Akasema, "Vema, nakwambia." Kasema, "Mchungaji wangu aliniambia ningeweza kufanya haya yote . . . " Naye alikuwa na rangi ya kutosha kupaka ghala. Vidole vya—vyake vilionekana kana kwamba alikuwa akila mnofu mbichi wa nyama ya ng'ombe huku makucha yake yamejaa damu.

Nikawazia, "Ewe mwanamke, huonekani kama Mkristo kwangu."

161 Sikiliza, mama, usiruhusu upuuzi wa namna hiyo ushindiliwe kooni mwako. Kisa kizuri cha ubatizo wa mtindo wa

kale wa Roho Mtakatifu kitaondoa huo kutoka kwako kama tu vile. . .?. . .Kweli. Kumbuka tu kwamba umerudi nyuma mahali fulani. Sijali yale mhubiri huyo mwanamke. . .Hakuteuliwa na Mungu, nitakwambia hilo kwanza. Hiyo ni kweli. Ni kinyume na Neno.

Sikilizeni. Hapakuwapo ila na mwanamke mmoja tu katika Biblia ambaye alipata kujipaka rangi apate kukutana na mwanamume, na huyo alikuwa ni Yezebeli. Mungu akamlisha kwa mbwa.

162 Kwa hivyo ukiona mwanamke amejipaka rangi. Unasema tu, "U hali gani, Bi Nyama-mbwa." Hiyo ndiyo Mungu alitengeneza kutoka kwake, maskini nyama ya mbwa tu. Kwa hivyo usizingatie hilo; hilo ni la ibilisi; kweli. Ambapo anapaswa kuwa: ajisafishe na kutenda kama. . .Kama vile Yakobo alivyomwambia mkewe na binti yake: "Jifanye kama unavyopaswa kuwa." Amina.

163 Tunachohitaji usiku wa leo, ni uamsho mzuri wa mtindo wa kale, wa Roho Mtakatifu, ukihubiriwa tena huku nguvu za Mungu zikiingia na kutoka miongoni mwa kanisa, na wanga na kola zikaondolewa. Haleluya! Naam, bwana. Hilo ndilo tunalohitaji. Naam, bwana, sawa.

164 Maskini Shamgari kule chini, yapata wakati alipojenga kitu, ndipo ikabidi jambo kama hilo kutukia. Hivyo ndivyo kanisa, wakati uamsho unapoanza, ndipo inabidi kitu kama hicho kuinuka. Ndugu, hubiri tu ninii za mtindo wa kale. . .

165 Naam, tulikuwa na kondoo wengi nchini mwetu. Nao walikuwa na mbwa wa kuwaua kondoo; tulimshika akiwa na sufu kwenye meno yake, tukachukua ile bunduki ya kale ya marisau, mitutu miwili, tukamlenga. Ndugu, hicho ndicho kitu cha kuwalenga jamaa kama hao ni bunduki ya kale ya marisau, mitutu yake yote miwili. Nawaambia, itanyosha mambo. Hakika itayanyosha; itazuia mauaji ya kondoo wako. Amina. Sikujua ningesema hivyo, lakini mnaweza tu kukumbuka hilo. Vema, wazieni hilo.

166 Jamani, na hapo, yapata wakati alipoingiza ngano yake ndani na kila kitu, hawa hapa Wafilisti wakubwa wanene wanakuja, wanapanda wakampokonye. Moja kwa moja wanakuja barabarani, wakamnyang'anye.

167 Siku moja, aliweka mazao yake yote ndani na yote yamepurwa. Huyo hapo, maskini huyo jamaa mdogo; akasimama kule chini kwenye ghala, alikuwa akitazama pande zote. Akasema, "Vema, mama, huenda labda tutaninii. . .tunaweza kuishi msimu huu wa kipupwe, sisi pamoja na hawa watoto." Akiangalia pande zote.

168 Ndipo muda si muda mwajua, akasikia kitu kikija barabarani, "Pump, pump, pump, pump." Hawa hapa wanakuja watu mia sita wenye silaha, wamevaa maskini helmeti

kubwa za shaba, viatu vyao vikubwa vya chuma, mikuki yao mikononi mwao, panga zao kubwa zikining'inia ubavuni mwao, wakipanda barabarani, wakamnyang'anye mazao yake.

169 Ninaweza kumwona maskini Shamgari akisema, "Loo, jamani. Angalieni kule. Hili hapa linakuja tena." Akamtazama maskini mke wake. Huyo hapo, viwiko vya nguo yake vimetokeza. Hao hapo watoto wadogo, wanaonekana wamekonda sana kwa sababu hawakuwa na chakula. Wafilisti walikuwa wamekichukua.

170 Hiyo ni kama vile Wakristo wengine wanavyoonekana usiku wa leo. Kitu kinachoonekana duni kuitwa mwaminio, Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Amina. Hana imani ya kutosha kutonesha herufi *i* kama ilikuwa ni wino. Hiyo ni kweli. Loo, jamani.

171 Msimwache ibilisi aje huku na kuondoa utukufu wa Mungu kanisani, na kumtuma mchungaji wenu huko akapate D.D. hizi zote na kurudi, na kusimama na kusema "amina" kama ndama anayekufa. Mnachohitaji ni dini ya mhubiri wa mtindo wa kale, ya huko msituni, ya anga-bluu, ya kuua dhambi, ambayo itahubiri ukweli na kusimama juu ya kile ambacho Mungu alisema kwamba ni kweli, na kuwakomboa watu. Amina.

172 Mimi sio mkorofi. Simaanishi kuwa, lakini ndugu wakati umewadia wa kuleta. . .kufanywa nyeusi, "nyeusi," na nyeupe, "nyeupe." Naam, bwana. Mtamleta Mungu katika kambi yenu, nanyi mtasikia kelele tena katika kambi ya Mfalme, mtakaporekebisha jambo hilo. Amina.

173 Sasa, angalieni. Na huyu hapa maskini mzee Shamgari alikuwa amesimama, akitazama nje dirishani, hawa hapa Wafilisti wanakuja. Kasema, "Loo, mamangu, angalia huko."

174 Maskini msichana wake mdogo akilia. Ninaweza kumwona akiweka mikono yake chini, akisema, "Baba, hatutakuwa na chakula chochote msimu huu wa kipupwe." Ndipo basi ninamwona mama, na hapo anaanza kulia.

175 Mnajua, Shamgari alitazama pande zote. Kamwe hakujua la kufanya. Akatazama pande zote. Akasema, "Nisingeweza kupigana. Mimi si mpiganaji, wala si—sina wakati wa kutoka, na kujifunza jinsi ya kupigana, na kufanya mazoezi haya yote na kadhalika. Si—sina wakati wa kufanya hivyo."

176 Lakini ilitokea aliangalia, hapo pembeni, palisimama maskini konzo la ng'ombe. Mnajua konzo la ng'ombe ni nini? Ni maskini fimbo kubwa yenye ncha ya shaba ya kugonga. . . kuwagonga ng'ombe waingie langoni, jambo la kwanza, na halafu kuchokora uchafu kwenye jembe walipokuwa wakilima nalo. Maskini konzo la ng'ombe limewekwa hapo, hicho ndicho kitu pekee ambacho angeweza kutia mkononi mwake. Lakini mnajua nini? Sisemi alikasirika, lakini hasira yake ya haki ilipanda. Naam, bwana. Ndugu, nitakwambia alifu-. . .

“Ni nini hiyo iliyo mkononi mwako?”

177 “Si kitu ila konzo la ng’ombe.” Naye akasema, “Mimi si mpiganaji. Si—siwezi kufanya hivi. Si—sina mafunzo yoyote.” Lakini hakuwa na wakati wa kufanya mafunzo yoyote. Kitu pekee alichohitaji ni Roho wa Mungu juu yake. Aliruka kutoka kwenye dirisha hilo akiwa na Roho wa Mungu juu yake na kunyakua konzo hilo la ng’ombe na kuwaua Wafilisti mia sita. Amina.

178 Tunachohitaji siku hizi, si kwenda kwenye seminari na kujifunza kama Marko 16 ni ya kweli au la. Ndugu, watu wanakufa. Jambo tunalopaswa kufanya ni kutoka sasa hivi. Sio kama utapigana au la; ni kusimama. Naam, bwana.

179 Alijua ya kwamba alikuwa Mfilisti. Alijua kwamba hao walikuwa ni Wafilisti wasiotahiriwa. Kwa hakika kama ninavyojua kwamba ugonjwa huo, maadamu unajua una shida ya moyo, hata shida yako iwe nini, tunajua ni ya ibilisi. Naye alijua ya kwamba yeye alikuwa Mwisraeli. Alijua ya kwamba alikuwa ametahiriwa. Alijua alikuwa na haki ya ile ahadi. Alijua ya kwamba Mungu angeahidi kumbariki. Kwa hiyo akashikwa sana na hasira yake, ndipo akanyakua hilo konzo la ng’ombe, akaingia kazini.

180 Tunachohitaji usiku wa leo, ni kuamini, ndugu yangu, kwamba wewe ni mtoto wa Mungu, nawe unayo haki kwake, na ahadi ni yako. Chochote kilichoko mkononi mwako, kichukue, anza kumshambulia ibilisi kutoka upande mmoja hadi mwingine. Amina. Nawe utaona ya kwamba manyoya yataanza kuruka, ibilisi atashindwa, nawe utatokea mzima tena.

181 Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Unasema, “Ndugu Branham, sina kitu mkononi mwangu.” Unaweza ukawa na kadi ya maombi. Angusha kitu hicho ardhini, na usimame katika Jina la Yesu Kristo, na useme, “Ninamchukua Kristo kama Mponyaji wangu usiku wa leo.” Haleluya!

182 Unaweza kuwa na katekisimo ndogo imetokeza mkononi mwako, huku ukitaka kunichunguza ujue kama ninasema kweli au la. Tupilia mbali kitu hicho, na usimame katika Jina la Yesu Kristo, na kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, kisha uende kambini. Amina. Naam, bwana. Huenda ukawa na lundo la kanuni ndogo za imani unazopaswa kukariri asubuhi kabla hujaenda kanisani, na ujifunze hizo, upate kuzikariri. Tupilia mbali kitu hicho na upate kujazwa moyo na Roho Mtakatifu. Amina. Angusha kitu hicho na uchukue kilicho mkononi mwako. Chochote kilicho mkononi mwako, kichukue, na ufanye nacho vizuri uwezavyo kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina. Masalale. Nilikuwa . . . Hili hapa, loo, karibu saa nne. Na tuombe.

183 Baba yetu wa Mbinguni, hakuna mengi mkononi mwetu; lakini Mungu si kile kilicho mkononi mwetu, ni kile Wewe unachoweza kuweka mkononi mwetu. Ee Mungu, tunahitaji

imani usiku wa leo. Chukua ujumbe huu mdogo usiku wa leo, Bwana, na uuweke moyoni mwa kila mwaminio, na uwajalie kujua kwamba haijalishi jinsi mtu huyo alivyo dhaifu, bado wana Kristo karibu. Nami ninaomba ya kwamba utatoa baraka hizi, kuokoa waliopotea, kuwajaza na Roho Mtakatifu wale walio nje ya Kristo, na kupata utukufu kutokana na ibada hii. Katika Jina la Yesu, ninaomba.

184 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nashangaa tunapofanya wito huu wa madhabahuni kwa muda kidogo tu. . . Najua haya ni mahubiri makali ya mtindo wa kale, yaliyosuguliwa, yakapunguzwa, ya kishamba yawezavyo kuwa, lakini ndugu unayahitaji wakati mwingine. Hiyo ni kweli. Unayahitaji.

185 Sasa, sijui kama kuna mtu yeyote hapa usiku wa leo, si mwenye hadithi ya kuhuzunisha apate kulia na kuendelea. . . Sikilizeni. Kutakuwa na watu wengi zaidi watakaodanganyika na hilo kuliko kitu chochote nikijuacho. Siendi Mbinguni kwa sababu mama yangu alienda huko. Ninaenda kwa sababu Yesu Kristo alikufa ili niweze kwenda huko. Nataka kumwona mama yangu, hakika. Lakini sina budi kuja kwa Kristo, si kwa sababu mama yangu alienda, bali kwa sababu nimekuja kama mwenye dhambi, naungama dhambi yangu, naikubali njia iliyoandaliwa na Mungu. Hiyo ni kweli.

186 Sasa, hivi wewe, usiku wa leo, unasema, "Mimi ni mwenye dhambi, mhubiri, na ninataka unikumbuke katika maombi. Ninainua mkono wangu kwako kuomba kwamba utanikumbuka katika maombi kama mwenye dhambi"? Je, utainua mikono yako, popote kusanyikoni? Mungu awabariki pande zote. Jamani, jamani, jamani. Juu kabisa kwenye ulingo karibu na ushoroba, je, kunaye mahali popote humo ndani? Naam, naona mikono yenu. Kote huko, Mungu anaiona pia. Hakika Yeye anaiona.

187 Mara baada ya ibada, nawatakeni mshuke mje hapa na kufanya maungamo, muutoe moyo wenu kwa Kristo, na kumtumikia Bwana kwa moyo wako wote.

188 Baba wa Mbinguni, usiku unapoendelea, watoto wadogo wagonjwa wameketi huku. Ninaomba, Mungu mpendwa, kwamba rehema Zako zitamiminwa katika mioyo yetu sasa hivi. Naomba somo hili dogo la *Ni Nini Hiyo Uliyo Nayo Mkononi Mwako?*. . . Kwa Musa, si kitu ila ni fimbo kavu; kwa Daudi, si kitu ila kamba mbili ndogo pamoja na kipande cha ngozi ndani yake, kombeo; kwa Samsoni, si kitu ila mfupa mkavu wa taya ya nyumbu (Ee Mungu!); Shamgari, si ninii. . . si kitu ila konzo la ng'ombe mkononi mwake, fimbo yenye kipande kidogo cha shaba nchani mwake, naye akawaua Wafilisti mia sita, si shujaa, si mpiganaji, bali mtu katika agano.

189 Ee Baba wa Mbinguni, hivi usiku wa leo, Bwana, hutamchukua kila mmoja mkononi Mwako? Lijalie, Bwana, na uifungulie imani mioyoni mwao, pia naomba Roho Wako Mtakatifu afanye mambo mengi kwa wingi sana usiku wa leo, Bwana, wanapongojea.

190 Jana usiku, nilifurahi sana kukuona ukiwafanya vipofu kuona, na viziwi kusikia, na wenye dhambi kuja Kwako. Na Ee Mungu, mambo haya yote makuu uliyofanya, waliopooza kukunjuka na kutoka kwenye viti hivyo, na kutembea huku na huko katika Jina la Bwana.

191 Ee Bwana Mungu, Wewe ni mkuu. Nasi tunakushukuru kwa ajili yake, na tunaomba ya kwamba utamwokoa kila mtu usiku wa leo anayeinua mikono yake. Jalia wasipotee kamwe, lakini jalia huu uwe usiku ambao watakupokea Wewe. Watu mia moja ama mia mbili hasa wameinua mikono yao, nami ninaomba ya kwamba utamwokoa kila mmoja wao kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa ni katika Jina Lake tunaomba. Amina. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

192 . . . Walituma Biblia milioni moja kwa Wayahudi hawa. Wamekuja hivi punde kutoka huko chini Iran kule, Iran, Iraq, na huko chini nchini kule. Mliyasoma, mkasoma kwenye hayo magazeti jinsi ambavyo ninii . . . walileta mamilioni ya Wayahudi. Tungekuwa na wakati wa kuingia katika jambo la kinabii . . . Na wale Wayahudi wanaorudi, nina picha yao wakiingia mle, mahali ilipopigiwa, wakitoka kwenye meli, wakitoka kwenye ndege, wakiwabeba walemavu wao, na viwete wao, na vipofu wao.

193 Basi wakawakaribia. Yule mtu aliyeipiga picha hii. Ndugu Arganbright na hao wengine, ambao wanatarajiwa hapa mkutanoni, alikuwa amewauliza, akasema, "Nyote mnarudi kwa sababu gani?"

"Ni nchi ya uenyeji wetu."

Kasema, "Ili mpate mahali penu wenyewe, mpate kufia kwenye nchi ya uenyeji wenu."

Wakasema, "Hapana. Tunarudi kumwona Masihi."

194 Loo, ninyi walimu wa unabii, laiti mngalijua hiyo ilikuwa ni nini. Wakati Injili hii itakapotoka kwa Mmataifa imwendee Myahudi, Mmataifa amekwisha. Ni wakati wa mwisho.

195 Na kwa hiyo wakawapa Biblia. Walituma milioni moja huko. Wayahudi hao wakaanza kusoma maagano hayo. Wakayamaliza. Kamwe hawakujua Yesu alikuwa hapa. Hawakupata kusikia lolote kuhusu jambo hilo, wamekuwa chini kule tangu ule uhamisho wa Babeli, utumwa. Nao wakasema, "Ikiwa huyu Yesu, mnavyomwita, ndiye Masihi, hebu na tumwone akifanya ishara ya nabii, jinsi alivyofanya hapa katika Biblia hii, nasi

tutamkubali. Sisi sote tutamkubali, kama atakuja na kufanya ishara ya nabii. Tutamkubali."

Ndugu, Loo, jamani. Nilikuwa katika maili mia kadhaa kutoka kwake majuma machache yaliyopita, lakini Roho Mtakatifu akanizuia, "Bado kidogo."

196 Loo, jinsi ningependa kuwakusanya wao milioni kadhaa, na kusema, "Ninatoa changamoto kwamba katika Jina la Bwana Yesu, kama hatafanya ishara ya nabii: ni wangapi wenu mahali papa hapa watamkubali kama Mwokozi binafsi?" Ndipo basi watakapofanya hivyo, nitasema, "Mahali papa hapa ndipo baba zenu wa mwanzoni walipoupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, na ishara zile zile alizofanya Yesu zitajirudia tena vile vile hasa mlivyoisoma katika Biblia."

Hawataki kuwa. . .Mungu wao ni Mungu mwenye nguvu. Mungu wao hafi. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, nao wanaamini hilo.

197 Angalieni. Yesu alipokuwa hapa duniani, hakudai kuwa mponyaji. Watu wengi walimjia ambao hawakuponywa. Mara nyingi labda alipelekwa kwa wafu. Nawazia kuna maelfu waliokufa alipokuwa hapa duniani. Hakuwafufua ila watatu; huo ni uthibitisho. Alipita kwenye birika la Bethesda ambapo watu walikuwa wamelala walemavu, viwete, vipofu na waliopooza, kamwe hakumponya hata mmoja wao, akamwendea mtu aliyekuwa amelala juu ya godoro, akamponya, akaondoka akawaacha hao wengine wamelala pale.

198 Mtu aliyejaa wema, aliyejawa na imani, Mungu Mwenyewe, Imanueli, hapa duniani, akiishi miongoni mwetu, Yeye alisema, "Sifanyi lolote Mwenyewe." Walipomwuliza katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo alitendalo Mwana vile vile." Sasa, yafuatilie Maisha Yake katika Biblia, uone kama haikuwa kila wakati yale Baba aliyomwonyesha. Yesu alisema, "Si Mimi nizitendaye kazi hizo, ni Baba Yangu akaaye ndani Yangu, Yeye huzitenda kazi hizo."

199 Wakati Filipo alipoongoka, akaenda akamwona Nathanaeli, akamleta, ilikuwaje? Alisema, "Njoo, umwone Yeye tuliye. . . Niliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu."

Akasema, "Laweza lolote jema kutoka Nazareti?"

200 Alipokuja kumwona Yesu, alienda mstarini kama huko nje. Yesu akamwangalia. Huenda alikuwa kwenye mstari wa maombi, nijuavyo mimi. Lakini akafika alipokuwa Yesu, akiwaombea wagonjwa. Akamwambia, alipomwangalia, Yesu alimwangalia, akasema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake."

Loo, akasema, “Ulipataje kunitambua, Rabi?” Akamshangaza.

“Mbona,” Yeye akasema, “kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

Akasema, “Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli.”

201 Akapanda kupitia njia ya Samaria. Alikuwa anaenda Yeriko, bali alipanda kuzunguka Samaria, juu kabisa ya kilima. Akaketi chini, akawatuma wanafunzi Wake. Mwanamke Msamaria akatokea. Alimwona pale akichota maji. Baba alikuwa amemwambia aende kule. Hakumwambia kile ambacho kingetokea, alisema tu, “Nenda huko juu.”

Kwa hiyo akamwona yule mwanamke pale, Naye akasema, “Nipe maji ninywe.”

Akasema, “Sio kawaida kwa Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho. Hatuchangamani.”

202 Akasema, “Lakini kama ungejua ni Nani unazungumza Naye, ungeniomba Mimi maji unywe.” Alifanya nini? Aliendelea na mazungumzo, hata akaishika roho yake; ndipo alipoishika roho yake, lililokuwa tatizo lake, akasema, “Nenda, kamwite mumeo.”

Akasema, “Sina yeyote.”

Kasema, “Umesema vema. Maana una watano, naye uliye naye sasa siye wako.”

Akasema, “Naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Akasema, “Sasa, najua ajapo Masihi, Yeye atafanya mambo haya, lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

Naye akakimbilia mjini, akasema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia yote niliyopata kufanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

203 Sasa, kama Yesu huyo ni Yesu yeye yule leo, angeweza kufanya jambo lile lile leo, na kadiri Mungu anavyofunua, Yeye anaweza kufanya jambo lile lile. Hiyo ni kweli?

204 Sasa, angalieni hapa jana usiku. Kulikuwa na wanaume na wanawake walioketi hapa chini katika safu hii, hapa, waliopooza, wameketi kwenye viti vya magurudumu. Usiku wa leo wako huko nje kwenye kusanyiko, popote walipo, wakitembea huku na huko. Kwa nini? Yesu Kristo.

205 Kulikuwako na wanaume, wanawake waliokuja jukwaani, dhambi maishani mwao. Roho Mtakatifu akashuka moja kwa moja, akawaambia tu ilikuwa ni nini na yale hawana budi kufanya. Waliponywa, wakiwa wamesimama pale pale jukwaani, wakatoa mioyo yao kwa Kristo. Ikiwa huyo si Yesu Kristo wa Biblia, siijui Biblia.

206 Mwasemaje wahudumu? Huyo anasikika kama Kristo wa Biblia? Sasa, si mwanadamu; ni Kristo. Sasa, kama Yeye atarudi usiku wa leo hapa, na kufanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani, je, ninyi nyote mtamkubali basi kama Mwokozi, kama Mponyaji, na kumwamini kwa moyo wenu wote? Kama mtamwamini, mtainua mikono yenu? Mungu awabariki.

207 Baba yetu wa Mbinguni, sasa ni, haya ndiyo yote nijuayo kufanya. Mengine ni Kwako, Mwokozi wangu mpendwa, nami naomba ya kwamba utatoa baraka, kupitia Jina la Yesu. Amina.

208 Sasa, tulichukua kadi zote za maombi jana usiku. Ninaamini walitoa mpya leo. Ikiwa yule mvulana . . . Naona alikuwa hapa kitambo kidogo kilichopita. Nazo zilikuwa nini . . .? O? Vema, hebu tuanze na tuwaweke mstarini baadhi yao, basi.

209 Ni nani aliye na namba moja? O, angalia kadi yako ya maombi na utaipata, kama upo, unaweza kuja huku. Je, mama huyu hapa . . .? Vema, naam, njoo tu huku juu, mama, papa hapa. Kwa namna fulani ni vigumu kidogo. Labda itabidi nimwite mmoja au wawili tu.

210 Ni nani aliye na O, namba mbili? Je, unaweza kuinua mkono wako, yeyote aliye na namba mbili? Mama huyo hapo nyuma, waweza kuja, mama, tafadhali? Ni nani aliye na O, namba tatu? Unaweza kuinua mkono wako? Yeyote aliye na O, namba tatu, unaweza kuinua mkono wako? Hapa nyuma, bwana? Samahani. Vema, waweza kuja huko juu? Namba mbili na namba tatu, sasa namba nne. Ni nani aliye na O, namba nne? Waweza kuinua mkono wako? Wewe, bwana? Je, waweza kushuka uje hapa? Sawa.

211 Namba tano. Ni nani aliye na O, namba tano? Unayo, mama? Waweza kushuka hapa? Namba sita, ni nani aliye na namba sita? Je, unaweza kuinua mkono wako? Namba sita? Baadhi yenu, bawabu, njoni hapa na m-. . ., au washike hawa hapa kwenye viti hivi. [Ndugu mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Vyovyote vile. Samahani.) Vema, hiyo ni sawa. Vema, namba . . . Ni nini mimi . . .? Tano? Nani . . . Sita? Ni nani aliye na saba? Kadi ya maombi ya saba, unaweza kuinua mkono wako moja kwa moja . . .? Saba, yule mama pale. Nane, unaweza kuinua mkono wako, haraka? Nane, tisa, unaweza kuinua mkono wako mara moja? Tisa? Vema, kumi? Na . . .

212 Sasa, wanapoingia mstarini. Sasa, ni wangapi katika kusanyiko hili, kila mahali sasa, ninataka kuwauliza. Sasa, mahubiri haya ya mtindo wa kale, ya kishamba yanaweza kuwa magumu jinsi yawezavyo kuwa, lakini, ndugu, hayo tu ndiyo ninayojua. Hilo ndilo lililoniokoa. Na hilo ndilo tu nijualo. Mimi . . . Yote nijuayo, sitaki kukuudhi, lakini hakika afadhali ningekuudhi kidogo sasa, nipate kukuweka sawa na Mungu; na ninajua itanibidi kusimama pale Siku hiyo, nawe utanielekezea kidole chako usoni mwangu, na kusema, “Kwa

nini hukuniambia ukweli?" Unaona? Ni afadhali nilirekebishe sasa, sivyo, kuyatatua yote?

213 Sasa, ni wangapi hapa hawana kadi ya maombi na wanataka kuombewa? Unaweza kuinua mkono wako? Inua tu mkono wako, usiye na kadi ya maombi, lakini hata hivyo unaamini ya kwamba Mungu atakuponya. Bwana Yesu katika rehema Zake akubariki milele. Vema.

214 Sasa, kama tutakuwa tu na kicho kwa muda kidogo, hebu tuone kama wako mstarini . . . Wewe . . . vema, kwamba, tuko wengi kadiri unavyoweza kuwaingiza kwenye mstari huo, nadhani. Vema, tutawaombea wachache hapa sasa, na kisha . . . Tutasubiri tu ki—kidogo tuone popote . . . Baba yetu wa Mbinguni wa thamani ataongoza. Sasa, ninawatakeni muamini kwa moyo wenu wote.

215 Naona mtu tayari amefika huku, huyo ni msichana wako? Ni wako? Mwanamume mmoja ana imani nyingi sana, ana msichana mdogo mwenye polio anayeketi hapa. Wakati mstari huu wa maombi unapoanza kuanza, yeye anashika hilo gango kubwa na kumtoa mtoto wake. Hiyo ndiyo njia. Hiyo ndiyo njia. Um-hum, na hiyo ndiyo—ndiyo imani. Hiyo ndiyo njia ya kuamini. Mwokozi wetu mwenye upendo anajua mambo yote, anaweza kufanya mambo yote.

216 Sasa, kwenye mstari huu wa maombi hapa, wachache tu, na labda tunaweza kusimamisha wengine wachache, katika muda mfupi. Nataka kuwaulizeni huko. Je, ninyi nyote ni wageni kwangu mlio katika mstari wa maombi? Kama ndivyo, inueni mikono yenu; ninyi nyote wageni. Ninyi nyote ni wageni huko nje? Inueni mikono yenu, kila mahali katika . . . Je, kuna . . . ? Wote ni wageni. Basi siwafahamu. Sijui lolote kuwahusu, lakini nataka kuwaulizeni kitu fulani. Tulifanye tu hili kwenye Biblia.

217 Sasa, vipi kama Yesu alikuwa amesimama hapa, amevaa suti hii aliyonipa? Sasa, vi—vipi kama alikuwa amesimama hapa? Angefanyaje na hali hii ya mambo usiku wa leo? Vipi kama—kama mtu huko nje angekuja na kusema, "Yesu utaniponya?" Unajua yale angekwambia?

218 Angesema, "Tayari nimekuponya. Huamini hilo?" Hiyo ni kweli? Yale aliyofanya pale Kalvari, hawezi kufanya tena. Mnaona? A—alikuponya pale Kalvari. Alikuokoa pale Kalvari.

219 Sasa unasema, "Niliokolewa miaka miwili iliyopita, Ndugu Branham." Kweli, hukuokolewa ninii miwili . . . Uliokolewa miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Uliukubali miaka miwili iliyopita.

220 Yesu alililipia dhambi zako alipokufa pale Kalvari. Alililipia ugonjwa wako alipokufa pale Kalvari. Kwa hiyo basi, ikiwa Mungu, katika rehema Zake, alifanya hivyo, jambo pekee angeweza kufanya sasa, ama, angechukua Biblia, ahubiri Neno. Ama, huenda akaweza kusema kwa lugha ambayo ingefasiriwa

na mtu mwingine na kumwambia mtu fulani jambo la kufanya. Ama, Yeye akiwa ni Mkuu wa manabii, angeweza, pengine, kusimama hapa kama alivyofanya katika wakati wa Biblia, nayo imani yako ingeweza kuja na kumgusa mpaka nguvu zingemtoka, naye angegeuka, aseme, "Ni nani aliyenigusa Mimi?" Naye angetazama pande zote na kukwambia kile hasa kilichotukia. Hiyo ni kweli? Je, huyo ni Yesu?

221 Basi kama mama huyu anayeketi hapa kwenye kiti angekuja hapa, naye Yesu angemjua, simjui. Mungu anajua hilo. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini kile ninachojaribu kuwaelezea, enyi marafiki, mpate kukumbuka sikuzote. . .

222 Sasa, Yesu alipofanya mambo hayo, Filipo alisema Yeye alikuwa ni nini? Mwana wa Mungu. Yule mwanamke alisema Yeye alikuwa ni nini? Masihi haswa, kwa sababu Yeye alifanya jambo hilo. Lakini Wayahudi walisema Yeye alikuwa ni nini? Kasema, "Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni ibilisi. Yeye ni Beelzebuli, mkuu wa wapiga ramli wote." Mnaona? Walijua Yeye alijua shida yao. Alijua mioyo yao. Alijua shida zao, kwa kuwa Baba alimwonyesha kile alichotaka ajue. Mnaona ninachomaanisha? Sasa, huyo ni Yesu usiku wa leo, yeye yule.

223 Vema, sasa, uwe na kicho popote ulipo, na sasa hili linapaswa kulitatua, mara moja milele.

224 Je, ungeweza kumleta mama huyo hapa, ama umwambie aje hapa? Njoo hapa. Ninaninii tu. . .Sasa, mama, nataka tu usimame hapo; hilo ndilo tu unalopaswa kufanya, ninii tu. . . Hilo tu ndilo ninalokuomba ufanye, kusimama tu hapo.

225 Sasa, sikujui. Hunijui. Umeinua tu mkono wako hunijui, wala mimi sikujui. Lakini Mungu anatujua sote wawili, dada, na Yeye, na Yeye. . .Nilisita kuhusu hilo "dada" kwa dakika moja, unaona, kusema hivyo, lakini ninatambua sasa ndivyo ulivyo. Sasa, unaona, ndilo la kwanza—jambo la kwanza najua kuwa wewe ni Mkristo, kwa maana mara nilipoishika roho yako, iliingia namna hiyo, ya kwamba ulikuwa Mkristo. Unaona? Roho yako ilikaribishwa. Kama iliendelea kuingia giza na mawingu, ningejua hukuwa; unaona, na kwa hiyo, nisingalikuita dada yangu. Kwa hiyo basi, lakini wewe ni Mkristo. Sasa, kiasi kile. . .

Sasa hivyo—sasa hivyo ndivyo Filipo alivyomwambia Nathanaeli.

Alipopanda kule, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli, au mwaminio, ambaye hamna hila ndani yake."

226 Akasema, "Ulijuaje nilikuwa Mwisraeli, mwaminio wa kweli?" Mnaona? Hiyo ni roho ile ile. Mwanamke huyo angeweza kuwa mwenye dhambi kupindukia, lakini ninajua yeye ni Mkristo. Mnaona? Kwa sababu jambo la kwanza, roho yake, wakati upako huu ulio hapa sasa, ilishika upesi sana. Mnaona? Niliona ilikuwa ni Mkristo, iliikaribisha. Mnaona? Hivyo yeye. . .Najua yeye ni Mkristo.

227 Sasa, kama simjui huyu mwanamke, yeye hanijui, kama Roho Mtakatifu atamfunulia kilichomleta hapa...? Sasa, bila shaka, kadiri ninavyozungumza naye, ndivyo angesema mengi. Mnajua hilo usiku baada ya usiku.

228 Lakini kama ingemwambia tu kile kilichomleta hapa, je, kundi zima lenu litaamini ya kwamba nimesema kweli? Hiyo ingekuwa ni Mungu akisema ni kweli. Sasa, mtu anaweza kupitia hapa na kukwambia jambo lolote ulimwenguni, ajiundie namna fulani ya ulokole, afanye lolote analotaka, kwamba... angeweza kufanya hivyo, kukwambia hivyo. Hilo haliifanyi kweli. Lakini Mungu anaporudi na kusema hiyo ni kweli, basi afadhali uliamini. Maana hiyo—hiyo...kutokuamini hilo ni dhambi.

229 Kwa hiyo nimeshuhudia. Sasa, ni wakati wa Mungu kushuhudia kama nimesema kweli au la. Vema, sasa, nimesimama tu hapa nikizungumza na huyu mama, sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini huyu mama anafahamu sana sasa hivi kwamba kitu Fulani kiko karibu naye ambacho si ndugu yake hapa, mwanamume. Kuna kitu Fulani karibu naye, ambacho anajua kipo. Na hicho ni Malaika yule mnayemwona kwenye picha. Yuko papa hapa sasa, Nuru tu kati yangu na huyu mwanamke. Hiyo ndiyo sababu ilishuka pale nami nikahisi makaribisho. Nuru kote kote, yeye ni Mkristo.

230 Sasa, nataka kuzungumza nawe kwa muda kidogo tu, kwa kuwa wewe ndiye mgonjwa wa kwanza. Nami ninataka kila mtu, haidhuru uko wapi na una shida gani, uangalie huku, na kusema, "Sasa, Bwana Yesu kama Wewe...Ninajua mtu yule kule juu, yeye ni mwanadamu tu. Na kama—na kama utaniruhusu tu, unijalie imani, na unijalie imani yangu ijengeke kufikia tu mahali kama vile ya huyu mama itakavyokuwa..." Na kisha uangalie yale Mungu atakayofanya, kisha umkubali Yeye kama Mponyaji wako ama kama Mwokozi wako, chochote unachohitaji.

Sasa, kuzungumza nawe, mama. Kuna watu waliotuzunguka karibu kotekote usiku wa leo. Sina budi kukutenga; roho kutoka kila mahali.

231 Sasa, mimi nikiwa mwanamume tu, halafu wewe ukiwa ni mwanamke tu. Ni picha ya aina ile ile tu ya Yesu akizungumza na yule mwanamke ki—kisimani. Ni mwanamume na mwanamke tena.

232 Sasa, sikujui wala sijapata kukuona, lakini lazima niitofautishe roho yako na roho hizi nyingine za watu wanaozungumza, ama, wanaoomba, wajua, kwenye wakati huu, imani ikiingia.

233 Lakini mara moja...Sasa, i—ikiwa kusanyiko bado wanaisikia sauti yangu, huyu mama ananiondokea, na yeye—yeye ni mama. Mwanamke huyo, ambaye amesimama mbele

yangu amekuwa hospitalini hivi majuzi, na hiyo imekuwa tu ni saa chache zilizopita. Alitolewa tu hospitalini leo hii, ama, alasiri ya leo; saa moja usiku wa leo, wakati alipotoka hospitalini. Ana ugonjwa wa nadra wa damu, pamoja na kuharibikiwa na akili. Nenda zako tu, dada, imani yako inakuponya, unajipa afya. Amina.

234 Unaamini? Moyo wako wote sasa, uwe na imani; usiwe na shaka. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana; lakini huna budi kuamini. Sasa, uwe na imani tu huko nje na utapata kile utakachoomba.

Maskini msichana anayeketi hapo amevaa koti la waridi akiwa na tatizo hilo la kibofu, umeninii tu. . .umeponywa. Mungu akubariki.

Weka mkono wako juu ya mama huyo aliye karibu nawe, maana anasumbuliwa na hali ya fadhaa, upande *huu kule*.

235 Baba yetu wa Mbinguni, imani yake iligusa. Nikawa dhaifu. Niliona Nuru Yako ikining'inia juu yake. Ninawatangaza wazima katika Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Amina.

Unaona, huhitaji kadi ya maombi. Kuwa na imani; amini kwamba Mungu amesema kweli. Kwani Yeye si kitu ila Kweli; Yeye ndiye chanzo cha kweli yote.

Sasa, iweni tu na kicho. Amini tu kwa moyo wako wote. Unapaswa. . .unaweza kupata u—ulichoomba ikiwa utaamini tu.

Sasa, huyu ni. . .? Huyu ndiye mgonjwa? Huh. Sijarukwa na akili, lakini ulimwengu kamwe hautajua, dada, ni hisia ya jinsi gani.

236 Sasa, ni. . .Ha—hatufahamiani. Hatufahamiani, nami ni ndugu yako katika Bwana Yesu, nasi tuko hapa tukijaribu kusaidiana. Kama ningeweza—kama ningeweza kukusaidia wala nisikusaidie, ningekuwa katili, kama ningeweza kukusaidia. Lakini hakuna kitu ndani yangu ambacho ningeweza kusaidia, isipokuwa Mungu anijulishe la kufanya. Kwa hiyo kama atanifunulia ni kwa nini umesimama hapa, utakubali, basi, kuwa ni kweli ikiwa ni fedha au chochote kile? Utaamini kwamba Mungu anavutiwa na kisa chako na atasikia? Utafanya hivyo?

237 Bwana anijalie, ndilo ombi langu, mnaponitazama. Sio, unajua kama vile Petro na Yohana walipopitia kwenye lango liitwalo Zuri walisema, "Tutazame sisi. Unaona? Tutazame sisi." Sio kuwatazama kana kwamba ni Yeye, bali kuzingatia tu yale wasemayo, kupata mvuto wa Roho.

238 Ninaona kwamba ulikuwa na tatizo la ugonjwa wa macho, nami ninamwona daktari anayeuchunguza. Naye akashauriana na mtu mwingine, na mtu huyo, hawajui macho yako yana shida gani. Hawajui. Hawawezi kuuelezea, kwamba ni nini. Na halafu,

ninawaona wakikupa kitu fulani hapa tumboni, ama chochote kile, ni tumbo lililoanguka. Una tumbo lililoshuka. Madaktari hao wamekukatia tamaa kwa sababu hizo. Na wewe hutoki—hutoki katika mji huu. Unatoka upande wa juu ya barabara *huku*: Atlanta. Naye huyo daktari alisema, "Binti Trudy," ama kitu kama hicho, alikuita. Hiyo ni kweli. Rudi nyumbani sasa na uwe mzima. Imani yako inakuponya. Mungu akubariki. Amini.

239 Wewe ndiye baba wa huyu mtoto? Mwamini Mungu. Usiwe na shaka, lakini amini, ikiwa unaweza kuamini . . . Sasa, kumbukeni, huyu si mimi. Msikieni; sio mimi. Sasa, mtazamo wako kwake . . . Liite utakavyo; hiyo itaamua utakachopata kwake. Inategemea jinsi unavyoliendea.

240 Yule mwanamke aligusa vazi Lake; nguvu zikamjia. Yule mtu aliyempiga usoni, na kumpiga kwa mwanzi, na kusema, "Tabiri useme ni nani aliyekupiga," hakukuwako na nguvu kwa hilo.

241 Ewe msichana, unayeketi hapo nyuma, unaumwa na kichwa, sivyo, mama? Unayeketi na kunitazama papo hapo, unaamini Ye- . . . ? Naam, mama, unaamini Yesu atakuponya? Kweli alikuponya papo hapo. Ninii yako . . . uliteseka na huo kwa muda mrefu, mama. Umekuacha sasa. Imani yako ilikuponya. Mungu aliye hai asifiwe. Loo, jinsi tunavyompenda. Jinsi unavyopaswa kumpenda.

242 Wakati Roho Mtakatifu anapojongea pale, kuna mtu ameketi moja kwa moja nyuma yako, ameketi pale akiugua yabisi kavu. Unaamini, bwana, ya kwamba Bwana Yesu atakuponya? Unaamini? Naam, bwana, unaamini? Vema, bwana. Unaweza kupokea uponyaji wako basi. Mungu akubariki. Kidogo linakushtua, sivyo?

243 Mwanamke anayeketi papo hapo nyuma, ameinua mkono wake juu, akiomba, ana shida ya kibofu. Anataka kuponywa pia, akinitazama moja kwa moja, ameketi moja kwa moja huko nyuma. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, huko nyuma, mama? Vema, kama unaamini, unaweza kupata uponyaji wako. Amina. Yeye si ni wa ajabu?

244 Mama, anayeketi papa hapa nyuma, moja kwa moja huko nyuma kupitia hapa, ananitazama moja kwa moja. Ninaona ile Nuru ikining'inia juu yake. Hana kadi ya maombi, lakini anaugua ugonjwa wa moyo na yabisi kavu. Nuru hiyo ilitoka moja kwa moja kwa mtu huyu hadi kwake, moja kwa moja kupitia hapa. Na sasa, dada, kama unataka kuamini kwa moyo wako wote, umevaa miwani, unataka kuamini, unaweza kuponywa. Yesu Kristo atakuponya. Mungu akubariki. Vema, hilo latosha. Um-hum. Amina. Uh-huh. Loo, ni ajabu jinsi gani. Unaamini?

245 Sasa, hapa, inaonekana kama mngeweza kuona jambo hilo, marafiki Wakristo. Mnaiona hiyo Nuru ikizunguka-zunguka? Amesimama papa hapa. Inakuja moja kwa moja juu ya yule

ma-. . . aliyeketi papo hapo, ambapo, una kuvimba kwa mishipa, unayeketi papo hapo. Unaamini Yesu atakuponya mishipa hiyo, akuponye? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Ikiwa unaamini, unaweza kupokea uponyaji wako. Mungu akubariki.

246 Samahani, bwana. Unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? U—umekuja na mtoto wako mchanga, mtoto mchanga mzuri sana. Sikujui. Unajua hilo. Mimi ni mgeni kabisa kwako. Sijawahi kukuona, nadhani, maishani mwangu, bwana. Hatufahamiani kabisa, lakini Mungu anatujua sote wawili, sivyo, bwana? Una mtoto wako mchanga, nami ninaweza kumwona mtoto huyo akitoka kuchunguzwa. Naye daktari anasema hakuna matumaini kwake. Mtoto huyo anaugua kansa kwenye damu, inayoitwa "lukemia." Hiyo ni kweli. Hakuna tumaini lolote ulimwenguni kwake.

247 Na ndugu yangu, baba ya mtoto huyo mchanga, unamhitaji Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wako, sivyo? Wewe ni mwenye dhambi. Je, utamkubali sasa kama Mwokozi wako? Wewe. . .Je, utainua mkono wako, useme, "Bwana, nakukubali"? Sasa, weka mkono wako moja kwa moja juu ya mtoto wako.

248 Mungu Mwenyezi, katika Jina la Yesu Kristo, sasa namkemea ibilisi huyu anayemwua mtoto huyu mchanga. Msamaha na neema na zimjie baba huyu, na jalia waende, na kuishi, na kushangilia pamoja, katika Jina la Yesu. Amina. Mungu akubariki. Dhambi zako zimetoweka. Mwamini Mungu sasa. Amina.

249 Mwamini Bwana Yesu Kristo na unaweza kuponywa. Je, unaamini?

250 Unaonaje, bwana? Je, unaniamini mimi kama mtumishi wa Mungu? Shida yako iko mgongoni mwako, ni ugonjwa wa uti wa mgongo. Hiyo ni kweli, sivyo? Una matumaini usiku wa leo kwamba unaweza kuokolewa, na jambo lingine, una tabia unayotaka ukombozi kwayo, sivyo? kuvuta sigara. Utaachana nazo sasa hivi? Inua mkono wako, useme, "Mungu, hii inaimaliza." Nenda zako, na ugonjwa wako wa mgongo utakwisha, katika Jina la Yesu.

251 Hebu tuseme, "Mungu asifiwe." Mauti yanakaribia, na maisha pia.

Je, unaamini kwamba Kristo angeweza kukuponya na pepo huyu mbaya sana? Unaamini atakuondolea na kukuponya kansa hii?

Mwenyezi Mungu, Mwanzilishi wa Uhai, Mpaji wa kila kipawa chema, tuma baraka Zako juu ya mwanamke huyu na umponye katika Jina la Yesu, ninaomba.

Shetani, nakukemea katika Jina la Yesu. Amina.

Nenda zako ukishangilia sasa.

252 Hebu kidogo. Unafikiri nini, bwana, uliyeketi hapo kwenye hicho kiti cha magurudumu? Je, unaamini? Unaamini Yesu atakuponya? Kidogo ilikugusa wakati huo, sivyo? Unatambua jambo fulani limetukia. Je, unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? Je, utanitii mimi kama nabii Wake? Basi unaweza kuinuka kutoka kwenye kiti chako cha magurudumu, na kukisukuma, uende zako nyumbani. Yesu Kristo atakuponya. Usiogope; amini.

253 Na nyinyi wengine, wakati akitoka. Mnaweza kufanya jambo lile lile. Huyo hapo, naam, bwana. Je, mnataka kusimama? Kila mmoja wenu simama kwa miguu yako kwenye wakati huu.

Mungu Mwenyezi, Mwanzilishi wa Uzima, Mpaji wa kila kipawa chema, tuma Roho Wako juu ya watu hawa, na uwaponye, kila mmoja.

Shetani, ninakuhukumu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo toka kwa watu hawa.

Kila mmoja wenu simama kwa miguu yako, kila mahali, na umpe Mungu sifa. Roho Mtakatifu . . .?. . .

55-0611 Ni Nini Hiyo Uliyo Nayo Mkononi Mwako?
Porter Stadium
Macon, Georgia Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org